MRADI WA WAFUNGAJI NGORONGORO

MBINU SHIRIKISHI ZA

KUJIFUNZA NA KUTENDA

Imeandaliwa na

John Rowley

Loserian Sangale

Table of Contents

Utangulizi **2**

1. Ushirikishi wa Kujifunza na Kutenda Ilikotoka **4**

2. Mchakato wa Ushirikishi wa Kujifunza na Kutenda (PLA) **6**

4. Misingi ya mbinu shirikishi **7**

5. Usaili **9**

6. Matumizi ya Ramani/ Michoro **13**

7. Michoro ya watu kuingia na kutoka kijijini **19**

8. Pia chati (Pie charts) **23**

9. Mchoro wa Chapati **25**

10. Mlinganisho (Ranking) **26**

11. Mlinganisho (Simple) **27**

12. Mlinganisho wa jozi - *Pairwise Ranking,* **29**

13. Mlinganisho sababishi (Matrix ranking) **31**

14. Mlinganisho wa hali ya maisha ya kaya (Well Being Ranking) **33**

15. Wadau - Stake holder Ranking **37**

16. Chimbuko la matatizo (Mchoro wa vyanzo na athari) **39**

17. Utatuzi wa matatizo **41**

18. Jedwali mlinganisho (Spectrum lines) **43**

19. Mchoro Unaobainisha uwajibikaji ni lini **43**

20. Force field Analysis **46**

21. The Prisoners Dillema **48**

22. Kalenda ya Msimu **51**

22. Kalenda ya Msimu **52**

23. Shughuli za kila siku **55**

24. Historia ya Jamii **58**

Utangulizi

Ingawaje nimekuwa nikitumia mbinu shirikishi katika kazi zangu na hata kutoa mafunzo kwa wengine kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita, sijawahi kutengeneza mwongozo rasmi. Nilisema kuwa kila mafunzo yaliandaliwa kwa malengo maalum na kwamba ingekuwa siyo sahihi kutumia materials yaliyoandaliwa kwa ajili ya mafunzo mengine ambayo yatatakuwa na lengo tofauti.

Nilisema kuwa ni muhimu kuwa na uwezo kunyambulika na kubadilisha mbinu shirikishi kufuatana na mahitaji. Kwa mantiki hii, isingekuwa ni vizuri kutengeneza mwongozo ambao utatoa maelekezo ya utendaji ambayo hayabadiliki. Kwangu mimi, jambo muhimu katika kuwawezesha watu wengine kutumia mbinu shirikishi (PLA) ni kwamba washiriki watajenga uwezo wa kutengeneza vielelezo vyao vya PLA na kuweza kuvitumia kufuatana na mahitaji mbalimbali yatakayojitokeza.

Kila nilipoendesha mafunzo ya mbinu shirikishi, kwa siku ya kwanza nimekuwa nikitoa kwa washiriki faili ambalo halina chochote, na kila siku ya mafunzo nimekuwa nikitoa kitini ambacho kinawekwa kwenye faili. Washiriki pia wanaweka kwenye faili taarifa zinazoelezea mazoezi na notes walizochukua kuhusu yale wanayojifunza. Kufikia mwisho wa mafunzo kila mshiriki atakuwa ametengeneza jalada lake lenye maelezo ya jinsi gani aendeshe PLA.

Nilishawishika kuanza kuandaa mwongozo huu baada ya kushirikiana na Loserian Sangale kuendesha warsha za PLA kwa wafanyakazi wa mradi wa ERETO uliopo Ngorongoro. Kwanza wafanyakazi wa ERETO walipendekeza kuwa ingekuwa ni msaada mkubwa sana kwao kama wangepata vitini mbalimbali ambavyo wamekuwa wakitumia katika mafunzo yao katika lugha ya Kiswahili. Ili kukidhi haja hii, ilibidi tuanze kuweka pamoja makaratasi mbalimbali yaliyotumika katika mafunzo ikiwa ni pamoja na baadhi ya yale ambayo washiriki waliyatengeneza wakati wa mafunzo.

Vile vile hata baadhi ya wafanyakazi wa ERETO ambao wamejenga umahiri katika kutumia PLA katika shughuli za mradi, nao pia wamekiri ya kuwa,itakuwa ni msaada mkubwa kama watapata tafsiri ya Kiswahili kama kitabu. Baada ya kuweka pamoja maandishi yote yaliyotumika kufundishia ilikuwa ni rahisi kuona ni nini kilichobakia ili kukamilisha kazi ya kutengeneza kitabu cha kutoa maelekezo ya mbinu za PLA. Tuliona kuwa kama watu ambao wana ujuzi mzuri wa kutumia mbinu za PLA wanahitaji maandishi ya kusaidia kuwaelekeza, hakuna sababu ya kukataa kuwandalia.

Kwa hiyo katika kitabu hiki kuna maelezo mengi yanayohusu matumizi ya PLA. Mbali na maelezo kuhusu nadharia, kuna mifano halisi kutokana na mazoezi ya PLA yaliyoendeshwa na wafanyikazi wa mradi wa ERETO katika maeneo mbalimbali yanayohudumiwa na mradi huu katika eneo la tarafa ya Ngorongoro kati ya miaka ya 1999 na 2002.

Bado tungependa kukiita kitabu hiki kuwa ni mwongozo kwa watumiaji wa PLA, ili kusisitiza kuwa imeandaliwa kwa ajili ya kuwasaidia watu ambao tayari wanafahamu kuhusu PLA na tayari wanatumia. Ingawaje kitasaidia kukupa mawazo, hakina majibu ya nini kifanyike kila wakati. Kwa kifupi ushauri ninaotoa ni kwamba “Itabidi ufikirie na kuamua mwenyewe ni nini kinafaa kufanyika kwa wakati wote”

1. Ushirikishi wa Kujifunza na Kutenda Ilikotoka

Kwa muda mrefu ilifikiriwa kuwa msingi wa maendeleo ni utatuzi wa kiteknologia kwa matatizo yanazikabili jamii. Ilidhaniwa kuwa kama watu maskini wakibadili technologia wanayotumia mambo yatakuwa mazuri. Kwa hiyo jambo ambalo jitihada za maendeleo zingelenga ingekuwa ni kubadilisha technologia ambayo watu maskini wanatumia na hali yao itabadilika. Usahihi wa mtazamo huu kwa muda wote uliendelea kupingwa.

Mwishoni mwa miaka ya 1960, na mwanzoni mwa cha miaka ya 1970, mitazamo ya maendeleo ilianza kuwa makini zaidi na haikuishia tu kutazama tecknologia peke yake. Utafiti kuhusu mitindo ya kilimo (Farming Systems Research) ilianza kutumia na kusifia manufaa ya kutafiti mfumo mzima wa kilimo badala ya mazao machache na mbinu za uzalishaji unaoambatana nao. Uchambuzi wa Kilimo na Ecologia (Agro- Ecological) ndiyo jina lililofikiriwa ili kuonesha kuwa utafiti unatazama ecologia (mazingira yote), ambayo ndiyo kilimo inategemea.

Hata hivyo jitihada nyingi za kuelewa ni nini kilikuwa kinatokea zilifanyika kwa kutumia utafiti ambao ulitumia dodoso kupata habari. Dodoso hizo ziliandaliwa na ukusanyaji wa habari kwa kuzitumia, ulisamamiwa na wataalam huku watu wa kawaida wakitakiwa kujibu masuali tu. Tazama baadhi ya sifa zilizotolewa kwa dodoso za utafiti. Robert Chambers alisema haya yafuatayo kuhusu tafiti hizi:

Dodoso

- Zinauliza maswali yaliyokwisha tayarishwa
- Maswali yanayoulizwa ni yale yale kwa wote
- Gharama kubwa kusaili watu wengi
- Uchambuzi wa kitakwimu unaweza ukachanganya kuhusiana kwa vitu kama moja ni sababu nyingine.
- Inakusanya habari nyingi na zote sio muhimu.
- Majibu yanarahisishwa sana
- Hazitambui kwamba ili kuelewa ukweli wa mambo unahitaji kuhusisha vitu vingi.
- Mtindo wa kuuliza maswali vilevile unamsukuma anyejibu kutoa majibu ya aina fulani

Tafiti nyingine hazikuwahi kuafanyiwa uchambuzi: dodoso kubwa la utafiti lapata kurasa 30 (linalouliza maswali ya fani mbalimbali kila fani ikiwa na masuali yake), na ambayo yakiulizwa hayatumii maneno maalum ya kurahishisha ufupisho wa majibu toka kwenye compyuta, na hata yanakitumika matokea ya ufupisho wake hayatolewi ili haitazamwi, na hata yakitazamwa hayafanyiwi uchambuzi na hata pale yanapochambuliwa na kuandikwa hayasomwi, na yakisomwa hayaeleweki na kumbukwa, na hata pale yanapoeleweka na kukumbukwa hayatumiki kubadilisha utendaji. Tafiti za hali ya vijijini bila shaka ni kati ya idara ambazo utendaji ni wa chini sana duniani.
Robert Chambers, 1981.

Utafiti Haraka na Shiriki (Rapid Rural Appraisal) ziliibuka miaka ya 1970 na mwanzoni mwa 1980 kama nyenzo mbalimbali zinazoweza kutumika kupunguza *upendeleo*, upotoshwaji*, na, ufujaji katika utafiti.* Nyenzo zinazotumika zinatoka kwenye nyanja mbalimbali lakini ambazo

zina baadhi ya vitu ambavyo vinafanana. Zinatumia vielelezo vinavyoonekana, na mlinganisho badala ya vipimo halisi na hii ilifungua uwezekano wa wanajamii kushiriki katika utafiti.

Utafiti Haraka Shirikishi ilikuwa ni ufunuo kwa wakereketwa wengi wa shughuli za maendeleo ambao waliona kuwa mbinu hii ilisaidia kutatua mengi ya matatizo yao. Kati ya taasisi zilizokuwa msitari wa mbele katika kusaidia uendelezaji Utafiti Haraka Shirikishi ni pamoja na IDS Sussex nchini Uingereza. Dhana za *kuuliza tuu kile usichokijua kabisa* (optimal ignorance) la kutakuta *usahihi unaowiana na mahitaji* (proportionate accuracy) zilikuwa na mvuto mkubwa sana na uliteka mawazo yao. Misemo kama vile *kuwaachia walengwa waendelee wenyewe* (hand over the stick) zilianza kukubalika katika majadiliano kuhusu maendeleo. Uwezekano huu wa kupambana na upendeleo katika majadiliano kuhusu maendeleo ulikaribishwa sana.

Kufikia mwisho wa miaka ya 1980 kulianza kuwa na hali ya kutoridhika na hali ya ***kuchota*** katika Utafiti Haraka Shirikishi ambapo wataalam walikuwa ndio bado wananasimamia mchakato mzima. Walikuwa wanatumia tuu mbinu bora zaidi za kufanya utafiti kuliko watafiti waliowatangulia. Utafiti Haraka Shirikishi ilielezwa kuwa ni njia ya kuwapa uwezo mkubwa walengwa wa shughuli za maendeleo. Idadi kubwa ya nyenzo za mpya za kuwezesha shirikisha zimekuwa zikiibuliwa na kujaribiwa na kwa viwango mbalimbali, ushiriki wa wanajamii imeonekana kuongezeka. Ikikuwa kana kwamba kuna mashindano ya kila mmoja kujaribu kuwa na ushirikishaji mkubwa zaidi kuliko mwenzake au mradi mwingine. Kwa kuwa eneo hili limekuwa na rutuba nyingi sana, lilianza kuibua nyenzo na mbinu mbalimbali ambayo zilipewa majina mapya.

Hata hivyo mambo umuhimu kuhusu kuwaachia/ kuwawezesha walengwa kufanya maamuzi na kuwahusisha makundi ambayo kwa kawaida yaliachwa pembeni katika maendeleo yamebaki katika akili za wanaharakati wa maendeleo na taasisi mbalimbali.

Ushirikishi wa Kujifunza na Kutenda ni mkusanyiko wa nyenzo na mitazamo na mawazo ambayo yametokana na mabadiliko mbalimbali ambayo tumeyaelezea. Tumechagua kutumia jina ambalo lilitumiwa kwa mara ya kwanza na taasisi ya IIED Uingereza kwa sababu inaelezea kwa vizuri zaidi kuliko majina mengine.

Kwa nini tutumie mbinu shirikishi?

Kuepuka upendeleo unaosababisha upendeleo au ubaguzi katika maendeleo:

- Kwa mfano
  - kuepuka tabia ya kwenda tu kwenye vijiji vyenye barabara nzuri tena kwa kipindi fulani cha mwaka.
  - Kuepuka kutembelea maeneo hayo hayo na kukutana na watu / nyuso hizo hizo.
- Tumia vyanzo vingi zaidi vya habari na kuboresha na kuhusisha watu na makundi mengi zaidi ya jamii.
- Rekebisha upendeleo na ubaguzi ambao umekuwepo
- Jali na kuthamini ujuzi na maarifa ambayo jamii inayo
- Kuepuka kuwa mtumwa wa maumizi ya dodoso ambazo zinawafanya watu wajisikie wamechoshwa
- Unapata matokeo ya haraka
- Unajenga ushirikiano mzuri

2. Mchakato wa Ushirikishi wa Kujifunza na Kutenda (PLA)

Tafsiri

- **Mbinu shirikishi** (Participatory Learning Action - PLA) ni mchakato ambao lengo lake ni kuwawezesha wanajamii kuelezea, kuboresha, kushirikiana, kuchangia na kufanya uchambuxi wa kina ambao unawawezesha kuandaa mipango na kutekeleza yale waliyopanga.

- Ni mtindo wa kujifunza wenye taratibu maalum, unaoweza kunyambulika kufuatana na mahitaji ambao inawawezesha wanajamii na wawezeshaju kujifunza kwa pamoja kwa manufaa ya jamii.

- Inatumia mbinu mbalimbali za mawasiliano na hasa zile zinazotegemea nyenzo zinazotumia; vielelezo vinavyoonekana kuliko maandishi au maneno na mlinganisho kuliko vipimo halisi.

Ushirikishi Katika Kujifunza na Kutenda ni mbinu ambayo kusaidia kufikia maamuzi ya pamoja kuhusu shughuli za maendeleo. Ni mchakato ambao msingi wake ni wawezeshaji wa shughuli za maendeleo kujifunza kutoka kwa na pamoja na na wana jamii, kwa kuchunguza, kuchambua na na kutathmini matatizo na fursa zilizopo na kufanya na kutumia kufanya maamuzi yanayohusu shughuli za maendeleo.

Matumizi ya mbinu za PLA
PLA inawawezesha watumiaji kutumia mbinu mbalimbali za kuchochea ushiriki wa hali ya juu wa wanajamii katika kuchunguza, kujadili, kuchambua na kufanya maamuzi yanayosukuma mbele maendeleo yao. Hata hivyo ili kutumia mchakato wa PLA kwa ufanisi, ni vizuri kuzingatia yafuatayo;

- Kwamba lengo la PLA siyo matumizi tu ya nyenzo zinazochochea ushirikishi, hizi ni mwanzo tuu wa mchakato ambao lengo lake hatimaye ni kuleta mabadiliko katiki hali ya maisha ya watu.

- Matumizi ya nyenzo hizi ni muhimu yaambatane na mjadala ambao unatafakari na kuchambua yale yaliyoibuliwa na wakati wa kujadili michoro, ili kuhakikisha kuwa sababu mbalimbali zilizotajwa pamoja na maelezo mengine ya jinsi gani, n.k.hayapotei. Majadiliano haya ni muhimu kuliko mchoro au mbinu iliyotumika kupata maoni hayo.

- Matumizi ya nyenzo ambazo zinaonesha bayana michoro au alama kuhusu kile kinachozungumziwa, na zinawezesha washiriki wote kuweza kuchangia kikamilifu bila kujali kama wamesoma au hajasoma.

- Mbinu shirikishi za PLA zinarahisisha uwekaji wa kumbukumbu kwa namna ambayo hata wale ambao hawakuwepo wakija wanaweza kuona nini kimezungmziwa na wanaweza kuongeza.

4. Misingi ya mbinu shirikishi

Inajumuisha mbinu na mchakato wa kujifunza kwa mtindo maalum ambazo kwa pamoja zinawawezesha washiriki wote (wanajamii na wawezeshaji) kujifunza kutokana na shughuli wanazofanya. Kwa kuwa mfumo huu wa kujifunza unategemea sana kufanyika kwa uchambuzi wa pamoja matumizi yake lazima yawa shirikishi.

Kusikia yasiyosikika kwa kawaida:
Mbinu nyingi za kujifunza kutoka kwa wanajamii zinategemea sana watu wenyewe kujitokeza. Hii ni kwa njia ya kushiriki katika mikutano, kujibu maswali, kukubali kusailiwa na jitihada nyingine za namna hiyo. Kuna sababu nyingi kwa kawaida zinazowazuia wanajamii wasishiriki. Mbinu shirikishi zinalenga kuongeza upana wa mawazo ya yanakusanywa toka kwenye jamii na kusikia sauti za wale ambao kwa kawaida hawasikiki.

Wazungumzaji ndio kawaida wanasikika.
Mikutano ya watu wengi, huwa kawaida ina watu ambao ni wazungumzaji wazuri na ambao hawazungumzi. Kama mkutano utatumia tuu mbinu ya mazungumzo wenye uwezo wa kujieleza watasikika na wasio na uwezo huo hawatasikika kabisa. Lengo la mbinu shirikishi ni kujifunza kutokana na mitazamo tofauti ya washiriki na kukwepa kujaribu kurahisisha hali halisi kwa kuipachika na tafsiri mmoja. Kila mshiriki anaheshimiwa na kutambulika kuwa ana mchango muhinu wa kutoa. Mbinu shirikishi zinatumia nyenzo mbalimbali ili kuhakikisha kuwa *mawazo na mitazamo mbalimbali* ya washiriki inasikika.

Wanajamii na wawezeshaji kufunza kwa pamoja.
Katika mchakato shirikishi ni muhimu kutambua kuwa kuna makundi kadhaa tofauti. Kundi moja kubwa ni la watu kutoka jamii/ kijijini, kundi kubwa la pili ni la watu kutoka nje ya jamii hiyo ambao ni wawezeshaji na washiriki wengine kutoka taasisi mbalimbali. Wakati mwingine katika kuchangia mawazo tofauti hizi zinaweza zikafunikwa kidogo lakini ni muhimu kuhakikisha kuwa mawazo ya wanajamii na yale ya washiriki wengine kutoka nje yanaonekana wazi ni yapi.

Wakati mwingine inakuwa ni muhimu kuwakumbusha washiriki kutoka nje kuwa maoni na msimamo wao sio lazima ichukuliwe kuwa ni sahihi. Wakati mwingine inabidi katika majadiliano kuwauliza washiriki maswali kuhusu chanzo cha imani fulani au maoni ambayo pengine siyo sahihi ili waweze kujiuliza ni kupi hasa ambacho wanakijua na wanauhakika nacho na ni kipi hawana uhakika na wanahitaji kuchunguza ili kupata uhakika.

Ni muhimi kuhakikisha kuwa mawazo na maoni yaliyotolewa yametoka wapi. Hatari ambayo ni muhimu kuikwepa ni ile ya kuchukua maoni ya washiriki kutoka nje ya jamii na kuwabandikizia washiriki kutoka ndani ya kijiji kwa kuwa hii inaharibu jitihada zote za kuhakikisha kuwa maoni ya wanakijiji yanasikika na kutumika kama msingi wa maamuzi kuhusu shughuli za maendeleo.

Washiriki kutoka ndani ya jamii kujifunza pamoja
Mbinu shirikishi zinajenga mazingira yanayoruhusu kubadilishana mawazo kwa hali ya juu kati ya washiriki kutoka nje na washiriki kutoka ndani na vilivile kati washiriki kutoka ndani wenyewe. Ni sura gani ambayo mchakato shirikishi itachukua, inatagemea sana malengo na makusudio toka mwanzo kuwa yale yatakayoibuliwa , yale ambayo washiriki watajifunza yatafanyiwa nini. Wakati mwingine washiriki wanachukua yale waliyojifunza na kuyapeleka

katika michakato mingine nje ya jamii. Mchakato wa namna hii huwa ni ya *kuchota* tuu na inakuwa na chine wa hali unaonekana kuwa wa hali ya chini zaidi na umuhimu wake kwa jamii ni mdogo zaidi kuliko ile michakato ambayo wanakijiji wanatumia yale waliyojifunza kwa michakato ya maendeleo yao wenyewe. Kutokana na umuhimu wa matumizi tofauti ya mchakato shirikishi, ni muhimu sana kuanzia mwanzo washiriki wajue madhumuni na makusudio ya matumizi ya yale wanayojifunza kutokana na mchakato huo.

Flexibility.
Siyo rahisi kupangilia kwa kirefu shughuli za mchakato shirikishi zitakwendaje kuanzia mwanzo. Ingawaje madhumuni yanapaswa kuwa wazi kuanzia mwanzo, kwamba mchakato utakwendaje, ni vizuri kungoja mpaka shughuli yenyewe ianze. Mchakato ufuate mizunguko ya kujaribu mbinu mbalimbali, upima matokeo na mafanikio yake na uandae mzunguko unaofuata kutokana na mafunzo uliyopata. Kutokana na umuhimu wa kuendelea kupima masomo yaliyotokana na sehemu hiyo ya mchakato, na kuandaa sehemu inayofuata, hii inaonesha kuwa muda wa mchakato shirikishi unaweza kuwa ni mrefu zaidi kuliko ule wa utafiti wa kawaida. Nadhani ni kwa msingi huu neno *"haraka"* limeondolewa kutoka kwenye jina linaloelezea mbinu shirikisho.

Nyenzo zinazotumika zinaweza kunyambulishwa kufuatana na mazingira, na mahitaji. Hii inarahusu kuwe na tofauti kidogo ya matumizi ya mbinu za PLA.

Kuhakiki kutoka vyanzo vingine.

Mbinu shirikishi zaidi hutegemea sana watu kuelezea maoni na mitazamo yao ambayo inahitaji kuheshimiwa na kutiliwa maanani. Hili ni muhimu sana kwa kuwa inapunguza umuhimu wa kutegemea vipimo vinavyotazama idadi kamili. Kwa kuwa mbinu shirikishi zinatumia maoni ya wana kijiji na vipimo vingine vya ubora, ni muhimu kujaribu kufuatilia kilichosemwa kama ni ukweli. Sehemu hii ya mchakato inaitwa kuhakiki ambayo inaashiria umuhimu wa kupata maoni kuhusu suala hilo hilo kutoka kwa vyanzo tofauti. Ingawaje ni tunaambiwa kuamini kila tunachoambiwa, ni muhimu kuhakiki ukweli wake kwa kina kwa kuuliza watu wengine. Washiriki waelewe jinsi ya kupanga kufuatilia wasiishie kuchukulia tuu wanayosikia kwa juu juu bila kufanyia uhakiki wa kina.

Mchakato wa kujifunza kwa pamoja
Masuala yanayozungumziwa siyo mepesi kuyaelewa na kuyaelewa na yanahitaji mijadala ya pamoja katika vikundi ili kuielewa vizuri. Ni vizuri kuwa na mchanganyiko mzuri wa washiriki ambao utaruhusu uchambuzi kunufaika na mitazamo mbalimbali. Mchanganyiko huu wa washiriki unaweza ukawa ni watu kutoka; taaluma mbalimbali, idara au sekta tofauti, kutoka nje ya kijiji (wawezeshaji) na wanajamii, na kutoka makundi mbalimbali ya jamii hapo kijijini.

Kuleta mabadiliko: Mchakato ambao ni shirikishi unazaa mjadala kuhusu matatizo, fursa zilizopo, na mjadala huu unabadilisha mtazamo wa washiriki kuhusu utayari wao wa kuanza kuleta mabadiliko. Kwa unatumia majadiliano na uchambuzi mchakato huu pia unasaidia kubainisha baadhi ya mabadiliko yanayohitaji kufanyika ili kuleta mabadiliko na Inawamotisha pia washiriki wafanye uamuzi kutekeleza yale ambayo yameonekana yanaweza kuboresha maisha ya wanajamii. Baadhi ya mambo ya kutekelezwa ni pamoja na kuimarisha uwezo wa taasisi kusaidia wanajamii katika jitihada zao.

5. Tufanyaje kuimarisha ya mbinu shirikishi

Iki kuimarisha ushiriki sehemu hii itajaribu kutoa maelezo ya kusaidia kuelewa kushiriki ni nini, kuangalia baadhi ya mambo yanayokwimisha ushiriki ikiwa ni kwa nini watu hawataki kusema ukweli. Haya yatatusaidia kutazama tufanyaje ili kuimarisha mbinu shirikishi.

Kushiriki
Neno kushiriki linatumika kwa namna mbalimbali na linaweza kuchukua sura mbalimbali. Ni vizuri kuelewa tuna maana gani tunapotumia neno kushiriki kwa kuwa mara nyingi tunasikia mara nyingi jitihada mbalimbali za kusaidia maendeleo ambayo zinadai kushirikisha wanakijiji lakini hatujui ni kiwango gani wameshiriki.. Hata katika miradi ambayo kilichofanyika ni kuuuliza tuu maoni ya wanakijiji, kuhusu maamuzi ambayo tayari yameshafanyika, hata nao wanadai kuwa jamii ilishiriki. Hii inatuaonesha kuwa kuna viwango tofauti za kushiriki kama inavyobainishwa katika jedwali.

Aina za kushiriki

Aina / kiwango	*maelezo*
1. Kwa kuelezwa au kutendewa	Wakijiji, jamii inaelezwa, Wanaletewa huduma bila wao kuhusika
2. Kutoa maelezo	Watu wanatoa maelezo pale wanapoulizwa
3. Kutoa maoni au ushauri	Watu wanatoa maelezo na maoni yao pale wanapotakiwa kufanya hivyo. Hata hivyo maamuzi yote yapo kwa wataalam ambao hawawajibiki kwa vyovyote kuchukua maoni ya watu na kuyafanyia kazi.
4. Kushiriki kwa makusudi maalum	Vikundi vinaundwa kwa madhumuni maalum na hii kwa kawaida inatokea baada ya shughuli kuwa zimeshaanza kwa muda na zinaundwa kwa msaada wa kutoka nje ya jamii. Baadhi ya vikundi hivi vinaweza baadaye kuja kujitegemea.
5. Kushiriki kunakotokana na kukubaliana kwa pande zote husika.	Hii inatokana na uchambuzi wa pamoja ambao unabainisha umuhimu na mipango iliyoandaliwa kwa pamoja. Vikundi vina sauti kuhusu maamuzi juu ya masuala yanayowahusu hapo kijijini. Jamii inaona kuwa kuna umuhimu wa kuendelea kuwa na vikundi pamoja na shughuli ambazo vikundi vinafanya.
6. Jamii yenyewe kuona umuhimu wa kuanzisha shughuli	Uamuzi wa kuanzisha shughuli umetokan na jamii kuona umuhimu wa kutatua hilo tatizo au hiyo kero. Kwa hiyo wanafanya uamuzi wa pamoja wa kuchangia na kuanzisha shughuli.

Kwa kutazama viwango hivi vya kushiriki inakuwa ni rahisi kuona kuwa pengine tunadai kwamba kiwango cha ushiriki cha mradi ni kwenye kiwango cha kukubaliana kwa pande zote husika wakati ambapo labda ipo kwenye kiwango cha kuelezwa tuu na kutendewa. Inawezekana pengine kiwango hiki kwa hakika kikafikiwa baada ya muda mrefu wa mradi kuendelea kushirikiana na jamii. Hata hivyo ni muhimu pia kutambua kuwa kiwango hicho cha juu siyo rahishi kukifikia iwapo mradi unahitajika uonyeshe matokeo haraka. Katika hali hii inakuwa ni vizuri kuwa wazi kwa jamii kuhusu viwango vya ushiriki vinavyoweza kufikiwa. i

Mapungufu ya Mbinu za Kushiriki

Mbinu za kushiriki nazo pia zina udhaifu wake ambao ni muhimu kuutambua ili tuweze kuona nini cha kufanya ili upungufu huu usiathiri ubora wa matokeo. Baadhi ya mapungufu muhimu yanayotajwa mara nyingi ni haya yafuatayo;

- Ni haraka na sahihi
- Nyenzo ni za haraka la mchakato unachukua muda mrefu
- Inaamsha mategemeo makubwa kutoka kwa jamii,
- Haitoi yaliyo majibu ya mwisho kwa matatizo
- Huwezi kusema haipendelei

Kwa nini wakati mwingine watu hawasemi ukweli

- Wanapenda kukuza wakifikiri kuwa ndiyo itakuwa nzuri zaidi.
- Kuona aibu
- Kuogopa kulipizwa kisasi
- Kuona kama anadhalilishwa kama vile anafanyiwa kila kila kitu.
- Wasiwasi kuwa majibu watanyia nini
- Kuona lugha inayotumika wanafanywa kama watoto wanaolelewa.
- Watakwambia unachotaka kusikia
- Swali lililoulizwa limewaelekeza wajibu hivyo
- Siku ilikuwa mbaya (au nzuri) kwake
- Hataki kuonekana mjinga
- Iki kutoonekana mjinga
- Kutoa jibu ambalo linakubalika
- Anafikiri kuna jibu sahihi na lisilo sahihi
- Anataka kumfurahisha msaili
- Hataki kumwambia mgeni maoni yake
- Kutojiamini (kwa kuwa hajahi kuuzwa swali hilo

Mfano Hai

Sababu kutoka zoezi la usaili katika kijiji kimoja cha mradi wa Ereto.

- Uaminifu, utiifu
- Swali liliuliza mambo ya ndani
- Kutokujisifia kwa mafanikio yao
- Kutojiamini
- Msukumo kutoka kwa wengine
- Kuhofia uwezekano wa kunyimwa mradi, kukosa fedha au heshima
- Kupata doa au sifa mbaya ya kudumu
- Kusema uwongo makusudi
- Kumjaribu msaili
- Kuonekana mzuri
- Kuogopa ukweli kujulikana
- Kuzoea kulalamika
- Siri
- Kubisha kutofautiana makusudi.
- Kutokuelewa dhamira ya swali kuulizwa.

Ukishaelewa kwa nini watu hawasemi ukweli, inakuwa ni rahisi sasa kujatazama nin kinaweza kufanyika kupunguza uwezekano wa kupata majibu yasiyo ya ukweli.

Tufanyaje matokeo ya mbinu shirikishi yaaminike zaidi.

1. **Uliza tuu kile usichokijua kabisa** ***(optimal ignorance):*** usikukusanye habari au taarifa bila kuchagua, amua ni habari ipi unahitaji kujua na ipi huhitaji kujua - usikusanye taarifa ambayo huhitaju kujua!

2. **Tafuta usahihi unaowiana na mahitaji (*proportionate accuracy*):** Usijaribu kuwa sahihi zaisi kuliko unavyohitaji kuwa. Mara nyingi unachohitaji pengine ni kuelewa mambo yanakwendaje, kwa mfano kujua kama hali inazidi kuwa nzuri au inakuwa mbaya au imekuwa mbaya kabisa inaweza ikatosha kuwawezesha kuhakikisha kuwa mambo yanarekebishwa.

3. **Tambua na kujaribu kurekebisha upendeleo na ubaguzi ambao umekuwepo:** Usijaribu kupata majibu ambayo ni wakilishi pale ambapo huwezi kupata sampuli kielelezo ambayo ni wakilishi. Ni muhimu kutambua na kukubali kuwa kila utafiti shikirikishi utakuwa na upendeleo fulani ama kwenye vyanzo au kwenywe maudhui na uwe wazi kuhusu upendeleo huo uliopo ni upi. Hii ndiyo sababu ni muhimu sana kuweka kumbukumbu kuhusu watoaji habari/ wasailiwa na washiriki wakubwa katika kila utafiti ni akina nani.
   Baadhi ya maeneo muhimu ambayo upendeleo maalum mara nyingi unakuwapo ni katika maeneo yafuatayo;
   - Upendeleo wa maeneo , mahali
   - Watu wanaochaguliwa kushiriki
   - Hadhi ya kijamii ya washiriki
   - Jinsia
   - Msimu
   - Heshima na taratibu zilizofuatwa

4. **Pima uhakika kwa kutunia vyanzo tofauti:** hakikisha hakikisha hakikisha! (*Nani alisema nini, Tutathibitishaje ukweli wa kile alichokisema? Je tumeshasikia mawazo hayo yakitolewa na mtu mwingine au mawazo yanayopingana au kutofautiana sana nayo ?*)

5. **Hakikisha kwa kutimia njia zifuatazo**

   - Shirikisha makundi tofauti/ mbalimbali
   - Tumia wawezeshaji/ watafiti tofauti
   - Mahali tofauti
   - Mrejesho ufanywe na wageni kwa jamii/ vikundi
   - Wageni wawaeleze wenyeji waliyoona na wajadili

6. **Mawasiliano wakati wa utafiti ama yawe nguvu na yachukue muda :**
   Uendelee kufanya uchunguzi sambamba: Ingawaje mchakato wa mbinu shirikishi unaweza ukatumia usaili mfupi mfupi, bado kwa ujumla unachukua muda mrefu. Katika kupindi ambacho unawasiliana na washiriki, inakuwa ni rahisi kupima na uhakika wa yale uliyosikia na kuona.

7. **Onesha tofauti na sio makubaliano au muafaka.** ***Fikiria mfano unaokanusha batililsha.***
   Tujiulize kama je tunaliachoambiwa siyo sawa? Nini kitanihakikishia kuwa nimekosea? Wakati wa mchakato shirikishi badala ya kujitahidi kukubaliana na wenzako tafuta njia za kutahadharisha kuwa pengine tumekosea ili muweze kutazama ni kiasi gani mnachosema kinatokana na yale mliyoona na siyo mnarudia yale ambayo tayari mnayafikiria siku zote.

8. **Kumbukumbu za Fikra (tazama kama mawazo yako yanabadilika) –** weka kumbukumbu ya fikra zako juu ya masuala mnayoyatafiti na pitia kumbu kumbu hizo mara kwa mara kuona kama yamebadilika. Njia moja nzuri ya kuonesha kama kuma ushiriki wa jamii umekuwa wa kiwango kizuri ni kutazama kiasi ambacho mawazo yako mwenyewe yamelazimika kubadilika. Mfano wa kiasi gani mawazo yako yamebadilika unaonesha kama kweli ulikuwa unasikiliza vizuri.

9. **Hakikisha kwa kuuliza wenzako:** Zungumza na wenzako katika ofisi moja au hata mashirika mengine kuhusu mawazo yaliyojitokeza kwenye utafiti uone nao wanasemaje.

10. **Washiriki kucheki - mkutano wa mrejesho na jamii**
    Hii ndiyo sehemu muhimu zaidi ya kupima usahihi wa yale mliyojifunza. Mawazo yenu ni vizuri yakarudishwa kwa vikundi ambavyo vilishiriki kujadili ili kuona kama mlivyoelewa ni sawa. *Je ni hiki mlichosema? Maana ilikuwa hivi ? Tulielewa kama ina maana hii, je ni sawa?*

Jinsi ya kudhibitisha matokea ya Utafiti shirikishi

- Tumia nukuu kutoka kwa washiriki
- Uwe na kumbukumbu ya washiriki wa kila mkutano na tarehe
- Idadi ya vikundi mlivyokutana navyo
- Vikundi wasailiwa tofauti wanatoa udhibitisho na ushahidi.
- Ripoti zilizoandikwa (*secondary sources)*
- Elezea msimamo wako
- Husisha viongozi
- Tazama kuna tofauti kati ya matokeo na takwimu kwa nini
- Taarika izingatie matokeo, iwe inasomeka, utumie vielelezo vilivyotimika.
- Mawasiliano mzuri na waliogharamia utafiti.
- Mrejesho kwa vikundi na jamii
- Mahusiano mazuri
- Tambua wahujumu na uwashughulikie

6. Usaili

Mahitaji ya usaili mzuri

Usaili mzuri unahitaji uzingatie yafuatayo;

- Maandalizi mazuri
- Masuali mazuri
- Matumizi mazuri ya nyenzo za PLA k.v michoro, mlinganisho n.k.
- Uwezo mzuri wa kufikiri
- Uchambuzi mzuri
- Mawasiliano yanayoonesha kuheshimu washiriki.

Heshima nzuri katika mawasiliano na washiriki

- Heshimu na kutunza wakati
- Eleza madhumini zoezi hili na uwe wazi
- Onesha unaamini ya kuwa yale wanajamii wanayoyafahamu ni muhimu.
- Onesha una imani ya kuwa mtajifunza mengi kutoka kwa wanajamii.
- Ishara za mwili wako uwe ni kielelezo kizuri (km unavyosimama,unavyokaa, unavyotama n.k)

Hakiki kilichosemwa kwa kutimua mbinu mbalimbali

- Uwasaili watu mbalimbali *(maswali hayo ili ufananishe majibu*)
- Uyasaili makundi mbalimbali (*wanaume, wanawake, vijana, wazee, vijiji*)
- Tumia mbinu tofauti kuuliza maswali (pengine hayo hayo)
- Tumia watu tofauti kuuliza (masuali hayo)
- Uliza maswali hayo katika maeneo na kwa nyakati tofauti

Mfano wa Usaili mzuri



Epuka maswali yaliyofunga Yanaweza tu kujibiwa kwa mkato Ndiyo au Hapana *(mfano: Mnatibu mifugo inapougua? Kama akijibu kwa kusema ndiyo au hapana, anafunga uwezekano wa kuendeleza mazungumzo).*
Itakuwa ni vizuri zaidi ukiuliza suali kama *mnaihudumiaje mifugo inapougua?*

Masuali yaliyo wazi Yanampa anayeulizwa uhuru wa kujibu kwa namna mbalimbali, ama kujibu kwa kirefu au kwa kifupi.

Epuka masuali yanayoelekeza Yanaelekeza jawabu linalotakiwa ni lipi na kumfunga anayeulizwa asijibu vinginevyo. *(mfano: si mliamua kutenga eneo hilo kwa malisho ya kiangazi?).* Badala yake itasaidia zaidi ukiuliza *Mnafanyaje kuhakikisha kuwa mifugo inapata malisho wakati wa kiangazi*?

Epuka masuali yenye sehemu mbili Lina masuali mawili au zaidi na anayehojiwa anaweza kuchagua ni sehemu ipi ya suali anataka ajibu.

(mfano: xxxxxxxxx)

Siyo wazi Anayehojiwa haelewi anachoulizwa na kutakiwa kujibu nini.

Maana zaidi ya mmoja Siyo wazi kinachoulizwa ni nini kwa kuwa suali hilo lina weza kuwa na maana zaidi ya mmoja.

Epuka masuali yanayoudhi: Masuali ya wazi yanayoyeza yakamuudhi msailiwa kwa kuhisi ama unamchimba sana undani wake, au kuna dalili za utovu wa adabu,k.m. *Wewe una umri gani? Uliacha kwenda shule ukiwa darasa la ngapi?* Bado unaweza ukapata maelezo ya masuali hayo kama ukiyauliza kwa lugha inayoonyesha heshima.

Tumia marafiki sita katika kuuliza masuali na kupata maelezo zaidi . Hili ni eneo ambalo kwa kawaida niligumu, na hasa pale inapojitokeza suala au vipengele ambavyo ni muhimu kufuatilia.

Nani, Nini, Kwa nini, Lini, Wapi, Vipi.
Katika kufuatilia suala ili kupata maelezo na kuelewa undani wake ni vizuri uwatumie marafiki hawa sita kwa kadri inavyowezekena kufuatilia.

Kwa mfano; Ni ***nani*** alifanya ***nini***? (mhusika na kilichofanyika)
Ni ***lini*** alifanya na ***wapi*** alifanya?
Kwa nini alifanya vile, ili apate manufaa gani au amnufaishe nani?
Alifanya ***vipi***, kwa kutumia mbinu, ujanja, au taratibu zipi? Alifanikishaje?

Masuala ya kuzingatiwa na wawezeshaji katika usaili

- Orodhesha masuala yote ambayo unatarajia yazungumziwe.
- Hakikisha kuwa kuna mgawano mzuri wa majukumu baina yenu wawezeshaji na mkubaliane kuhusu ishara mtakazotumia baina yenu wenyewe.

- **Elezea vizuri ninyi ni nani na malengo yenu** kwa kuwa washiriki watataka kujua ni mlichokufuata ni nini.
- **Eleza wazi kuwa usaili utachukua muda gani.**
- **Angalia mazingira ya mahali unapofanyia usaili kama panafaa, na kama washiriki wote wanachangia kikamilifu.**
- **Uelewe vizuri ni nini hasa unataka washiriki wajadili** na ni kwa nini mnataka kujadili masuala hayo.

- **Uliza masuali yaliyo wazi** kama vile (nani, nini, kwa nini, lini, wapi, vipi)
- **Uliza upate maelezo zaidi** usiridhike na jibu la kwanza au jibu la mkato.
- **Pima kila unaloambiwa** kama ni; ukweli, uvumi, au maoni binafsi ya mzungumzaji.
- **Usipendelee upande wowote kwa kuonesha** wazi hisia zako kuhusu majibu yao. Amini unachoambiwa lakini ni muhimu uifanyie utafiti zaidi ili ufahamu undani na ukweli wake.

    - **Rekebisha na kuboresha mbinu/ nyenzo unazotumia kufuatana na mazingira**

    - **Kila mhamasishaji aachiwe akamilishe sehemu ya masuali ambayo anayauliza.**

    - **Hifadhi kumbukumbu**

- Kama itahitajika, andika majina ya washiriki wote
- Uelewe vizuri ni aina gani ya washiriki wanahitajika ili uweze kupata maelezo sahihi kuhusu masuala yanayouliziwa
- Hamishia michoro kwenye karatasi (*inapowezekana washiriki wenyewe wahamishe) Unaweza pia ukapiga picha.*

- **Hakikisha washiriki wanachangia kikamilifu.**

- Tegemea kwamba wakati mwingine utakuwa na usaili hafifu. Ikitokea hivyo uwe tayari kubadili na kufanya shughuli nyingine kwa kipindi hicho.

- Tegemea kwamba wakati mwingine kunaweza kuwa na hujuma na uweze kuigundua.

- Tumia lugha rahisi na inayoeleweka. Epuka matumizi ya maneno magumu ambayo washiriki hawayafahamu.

6. Matumizi ya Ramani/ Michoro

Michoro na ramani ni njia moja inayosaidia kupanua namna watu wanavyoweza kuwasiliana. Inawawezesha washiriki kuelezea mawazo yao kwa maneno ambayo mtu asikia bali pia kwa michoro ambayo mtu anaiona na kuelewa vizuri zaidi kile kinachozumgumziwa. Michoro na ramani inapanua uwezo wa washiriki kujadili na kuchangia katika mada inayozungumziwa.

Yanayojadiliwa kwa kutumia ramani na michoro yanahusu vipengele mbalimbali vya masuala ya kimazingira, kiuchumi, kijamii, utamduni na taasisi mbalimbali ambazo ama zinaonesha fursa au matatizo mbalimbali yaliyopo. Kuchunguza na kuelewa vizuri vipengele hivi kunasaidia washiriki kutoa ufumbuzi ambao utakuwa ni endelevu, na unaozingatia haki sawa katika jamii.

Kwa nini michoro?

- **Ni rahisi**
- **Inatumia maneno, tafsiri na mawazo ya jamii husika**
- **Ni kitovu cha majadililiano**
- **Inarahisisha ushiriki na uchambuzi wa washiriki (kwa kawaida wasemaju wazuri ndio wanasikika)**
- **Inarahisisha uulizaji wa maswali**
- **Inawapa sauti/ uwezo wa kuamua**
- **Inafurahisha**

Madhumuni

- Kujifunza kuhusu jamii na asilimali mbalimbali kwenye jamii. Mkazo siyo kupata mchoro sahihi, kivipimo bali ni kuelewa maoni ya washiriki kuhusu asilli mali na hata upatikanaji wa huduma za kujamii.
- Kurahisisha uchangiaji mawazo wa washiriki wote kwa kiwango sawa bila kujali kama amesoma au hajasoma.
- Zinawawezesha washiriki wote kuchangia kuhusu; asilimali, matatizo na fursa zilizopo.
- Zikishanakiliwa katika karatasi, ni chombo kinachoweza kuendelea kutumika mara nyingi na washiriki kuendesha mazungumzo kuhusu masuala ya maendeleo.
- Ni mojawapo kati ya mbinu rahisi na za kwanza zinazoweza kutumika kuelewa masuala muhimu kuhusu eneo la utafiti.

Aina za ramani

Ramani zinaweza zikaonyesha rasilimali, huduma mbalimbali, na hata masuala masuala kuhusu makundi mbalimbali ya kijamii kama ifuatavyo;

- Asilimali k.v, maeneo ya malisho, misitu, milima, mito, mapori, vyanzo vya maji, mabonde, n.k
- Miundo mbinu zilizopo kijijini, huduma mbalimbali za kijamii, k.v huduma za afya, shule, masoko, maduka, vituo vya usafiri, sehemu za ibada, nk.
- Mashamba, maeneo ya bustani, mazao mbalimbali, nk
- Masuala kuhusu makundi mbali mbali ya kijamii (social groups) kama vile; idadi ya kaya, maeneo ya kaya maskini, kaya zenye; uwezo, wajane, watoto walioacha shule, wagonjwa wa muda mrefu, wasio na uwezo, wenye watoto ambao hawajapata chanjo, n.k.
- Kwa ramani za makundi mbalimbali ya kijamii (social maps) kama idadi ya kaya zinazoorodheshwa ni nyingi, itakuwa ni vizuri kuendelea kuorodhesha kwenye karatasi, baada ya kuridhika kuwa washiriki wameshaelewa lengo la zoezi, na wataendelea kuchangia bila matatatizo.

Mbinu
Chagua eneo lenye na lenye udongo au mchanga laini na ambalo lina nafasi ya kutosha washiriki kukaa na kuchora chini.

Waeleze washiriki kwamba unataka kujifunza kutoka kwao kuhusu eneo lote la kijiji chao. Ili kurahisisha zoezi hili, washiriki wachore picha ya eneo lote ka kujiji chao kwa kutumia vitu muhimu vinavyoonesha mipaka ya kijiji k.v. mito, milima, nk.

- Mpe mshiriki mmoja kijiti aanze kuchora mipaka ya kijiji inakopita na washiriki wengine wawe wanachangia mawazo au hata wampokee ili kuhakikisha kuwa ramani inayochorwa inaonesha mipaka yote na njia kuu za kuingia na kutoka kijijini. Washiriki pia wanaweza kupanga mawe madogo madogo, kutumia majivu au kitu kingine kinachoweza kuonesha vizuri eneo la kijiji.

- Baada ya kubainisha mipaka, washiriki waendelee kuonesha kwenye ramani maeneo muhimu ya malisho kwa mifugo kwa misumu mbalimbali , vyanzo vya maji, huduma za afya, maeneo ya ibada, maduka, mashine ya kusaga na maeneo mengine yaliyo muhimu kwao.

- Tumia vitu vinavyopatikana hapo kama vile mawe, vijiti, majani mabichi au makavu, kinyesi cha mbuzi, ng'ombe, miiba n.k. kuonesha vitu mbalimbali.

- Washiriki wengine wachangie kwa kuongeze vitu vingine muhimu ambavyo bado havijaoneshwa.

- Tazama na kuwahimiza washiriki wote kuchangia mawazo kwenye uchoraji wa ramani kikamilifu.

- Mwezeshaji asikilize maelezo yanayotolewa kuhusu ama rasilimali, miundo mbinu, au huduma, kwa iuangalifu. Ni vizuri kupata sababu zinazoeleza k.m.nani, kwanini, wanatumia mbinu zipi, nk.

- Pata maelezo zaidi kuhusu maeneo ambayo huduma au vitu mbalimbali vinaoneshwa.

- Hamisha ramani iliyochorwa kwenye karatasi. Hakikisha ramani imewekewa ufunguo wa kuonesha ishara zilizotumika zina maana gani ili iwe rahisi kwa watumiaji wengine ambao hawapo hapo kuielewa.

- Kama ikiwezekana washiriki wabakie na nakala ya ramani waliyotengeneza.


KIJIJI CHA KAKESIO
UFUNGUO
Mabama
Shamba
Mbuzi
Bambam
Mito
Mto na Ormchem
Mipaka
Mambo ya kale
Shule
Hori la kunywesha mifugo
Dipu
Crush
Ofice ya kijiji
Maeneo ya Malisho
Ormchem ya Ebore
Shule
Mto wa Nkiri
Engeshey
Lengidang'a
N
W
E
S

7. Michoro ya watu kuingia na kutoka kijijini

Mojawapo kati ya matumizi ya michoro au ramani ni kusaidia kubainisha masuala yanayohusu upatikanaji au kutopatikana kwa huduma mbalimbali katika jamii. Watu wanaingia kutoka nje kufuata huduma na fursa, vilevile wanajiji wanatoka kwenda nje ya jamii kwa kuwa kuna huduma na fursa wanazofuata. Zote hizi zina faida na athari ambazo inaleta kwa jamii ambazo zinahitaji kutazamwa.

Madhumuni

- Kuonesha jinsi watu wanavyoingia na kutoka kwenye eneo/ kujiji. Zinasaidia kubainisha kuwa ni nani anaondoka au kuingia, wanakwenda toka wapi, na sababu ya kuondoka au kuja.

- Mbali na kuweka kumbukumbu, michoro hii inasaidia kuchambua na kufananisha na makundi mbalimbali katika katika jamii hiyo yana mawasiliano gani na jamii nyingine.

- Kuonesha ni mambo gani yanawafanya wana kijiji watoke kwenda maeneo mengine na ni nini kivuta watu kutoka maeneo mengine waje kwenye kijiji hiki.

- Kubainisha kiasi cha muda unaotumika kutembea kutoka sehemu moja kwenda ingine.

Mbinu

- Eleza washiriki kuwa lengo la zoezi ni kufahamu wanakijiji wanatumiaje muda wao, na ni nani anaingia na kutoka ndani ya kijiji.

- Anza kwa kuanzisha mjadala kuhusu mambo mbalimbali ambayo yanasababisha wanakijiji kutoka nje ya kijiji na wengine kuingia kijijini kutoka nje.

- Mwambie mshiriki mmoja achore duara kwenye udongo ambayo itawakilisha kijiji.

- Washiriki wapokezane kuweke mishale inayoonesha wanakijiji kutoja nje ya kijiji au watu wa nje kuingia kijijini. Kila mshale unapowekwa kumbuka kuuliza kwa ni akina nani wanatoka au wanaingia kijijini na ni kwa sababu gani? Uliza pia kama hali ya watu kutoka na kuingia imekuwa hivi tangu zamani au ni hivi karibuni tu imeongezeka (au imepungua)

- Uliza wanakijiji wanaume na wanawake wakitoka kijijini ni wapi hasa wanakwenda. Ni kwa nini wanakwenda na wanakwenda wapi. Washiriki waoneshe majjibu kwa kutumia ama mawe, majani, vijiti au alama nyingine yeyote inayofaa.

- Rudia kuuliza suali hilo kwa ajili ya makundi mengine ya jamii hapo kijijini na hata kwa watu wanaoingia kutoka kijijini kutoka nje uangalie kama majibu yake ni tofauti.

- Uendeleze mjadala kuhusu watu wanafanya nini ni kama wanafanya hivyo mara kwa mara. Uliza kama; vijana kuhamia mijini, au wanawake kusafiri kwenda vijiji vya jirani kufuata huduma za afya ni nzuri au mbaya na kwa sababu gani.

- Baada ya kukamilisha mchoro washiriki wajadili nini wamejifunza kutokana na zoezi hilo.

- Washiriki wahamishie mchoro huo kwenye karatasi na kuwe na nakala ya kubaki kijijini.

Maswali yatakoyosaidia wakati wa kutengeneza mchoro;

- Makundi mbalimbali yanakwenda wapi ndani na nje ya kijiji? Kwanini, lini, na mara ngapi?
- Kutoka nje ya kijiji ni nani wanakuja? Wanatoka wapi? Wanafuata nini? kila baada ya muda gani na wanakaa kwa kipindi gani?
- Ni nini uzuri au ubaya wa watu kutoka na kuingia kijijini mara?

Kijiji cha Olodung'oro

1. Watu wanaotoka wanakwenda wapi



2. Watu wanaoingia watoka wapi



3. Vitu gani Vinapelekwa nje



4. Vitu gani vinavyoingizwa kijijini



Mchoro wa watumiaji wa bwawa la Alaltaana- Ooudo



Maelezo:

- Watumiaji wengi zaidi wanatoka Ingereyani kuliko vijiji vingine kwa kuwa wanatumia kwa msimu wa masika na kiangazi.
- Watumiaji wa kutoka Ingarusi ni kwa kipindi cha kiangazi tu.
- Vijiji vya Ingereyani, Orgumiy na Esere wanahamisha mifugo yao kupeleka Ingarasu wakati wa msimu wa kiangazi halafu wanatumia bwawa hili.
- Katika miezi ya January hadi April ambacho ni kipindi cha mvua nyingi, vijiji vya Orgumiy Esere na Ingarusi havitumii bwawa kwa kuwa kwani wanapata maji kwenye maeneo ya karibu.

Watumiaji wa Chemchemu ya Esere



8. Pia chati (Pie charts)

Madhumuni
Pia zinasaidia kubainisha ukubwa wa tatizo au jambo linalozumgumziwa kwa namna mbalimbali kama ifuatavyo;

- Kwa kufananisha kundi la vitu katika kipindi kimoja na kuona ni kipi kikubwa zaidi. Mfano kufananisha magonjwa mbalimbali ya mifugo kv *oltikana, orkipei, ormilo,* na *emburwo* ili kuona ni ugojwa upi ambao uliathiri mifugo mingi zaidi katika kipindi kinachozungumziwa (tazama mfano ukurasa unaofuata).
- Kwa kufananisha kundi moja au makundi ya vitu katika nyakati mbalimbali ili kujua ukubwa na kuona tofauti. Kwa mfano ukifananisha ukubwa wa mvua, upatikanaji wa maji ya kunyweshea mifugo katika, ukubwa wa athari ya mifugo kutokana na magonjwa, n.k. Inawezakana kufananisha vitu hivi kwa kutumia pia inayoonesha ukubwa wa magonjwa haya katika vipindi mbalimbali.
- Inaruhusu kufananisha kwa haraka hali ya tatizo linalozungumziwa (uchache au wingi) katika vipindi mbalimbali na kuona jinsi gani linaongezeka na kuhusisha na athari kwa jamii.

Mbinu
Ama kwa kuandika chini kwenye udongo au kwenye karatasi kubwa (flip chart), andika vipindi unavyojadili (inaweza kuwa ni miezi, miaka, miaka miwili miwili au mitano mitano n.k.0 kama kama washiriki watakavyoona inafaa kwenye upande wa kushoto.

Jadili ukubwa au uwingi wa kile kinachozungumziwa na mkubaliane ukubwa wa duara litakalowekwa kuwakilisha tatizo. Kama ni kwenye karatasi chora duara au kata duara la karatasi ya rangi kiasi kinachowakilisha ukubwa wa tatizo na ukibandike upande wa kulia wa pale tatizo lilipandikwa.



Pia ya magonjwa mifugo kijiji cha Endulen 2000

1.



Ormilo	*Oltikana* ECF	*Orkipei* CBPP	*Emburwo* Chambavu Black Qurter

Pia hizi zilizochorwa na kikundi kimoja zinabainisha kuwa ungonjwa wa Ndigana ndio ulioathiri mifugo zaidi kwa kipindi cha mwaka huo.

Pia ya mvua na athari ya magonjwa ya mifugo kijiji cha Esere 2000







9. Mchoro wa Chapati

Madhumuni:

- Kuchunguza na kupata kujua kuhusu shughuli za asasi mbalimbali zilizopo kijijini, aina za shughuli wanazoendesha na umuhimu wa shughuli na asasi hizi kwa washiriki. Hii itaonekana kutokana na jinsi ambavyo washiriki watazipima na kuamua kuwa ni ipi ina umuhimu mkubwa zaidi kwao na kwa nini.

- Kubainisha na kujadili maoni ya washiriki kuhusu asasi hizi mbalimbali zinavyohusiana katika utendaji wao wa kazi.

- Kubainisha mapungufu katika mawasiliano, maeneo yenye msuguano wa kutokuelewana, na mianya ya nafasi za maendeleo zinajitokeza.

- Kufahamu ni asasi zipi ambazo zinaheshimiwa zaidi na washiriki, na hizi zinaonesha uwezekano mkubwa wa kushirikiana nazo.

Mbinu

Uliza kuhusu asasi mbalimbali zinazoendesha shughuli hapo kijijini (hizi ni pamoja na idara za serikali, shule, vikundi vya kujitegemea, mashirika ya hiari, madhehebu nk). Washiriki wafafanue mahusiano yaliyopo kati yao na taasisi hizi.

Ulizia kuhusu jinsi ambavyo taasisi na mahusiano yao yamebadilika.

Hakikisha kuna nafasi ya kutosha kuchora chini michoro ya ukubwa mbalimbali. Kama itataamua kutumia michoro ya duara kwenye karatasi inayohamishika kwa urahisi, hakikisha unayo ya kutosha na ya ukubwa mbambali.

Wape washiriki waanze na kuchora asasi walizoanza kutaja.

Waambie wauendeleze huo mchoro kwa kwa kuonesha ni jinsi gani taasisi mbalimbali zinahusiana.

Chagua mifano ya kuonesha kuwa kuna kuingiliana kwa shughuli, au mahusiano mazuri, dhaifu au pale ambapo mahusiano yapo kabisa.

Ulizia kama kuna makundi au asasi ambazo zinafaa kuingizwa katika mchoro wa chapati hata kama hayana mahusiano na mengine.

Ulizia kuhusu mahusiano ambayo hayaonekani kuwa ni wazi.

Usiweke mambo mengi sana ndani ya mchoro wa chapati. Mchoro wa chapati mara nyingi ni mgumu kuelewa kuliko ramani. Wasaidie washiriki watengeneze michoro yao na kama wakiamua kutumia misitari kuonyesha mahusiano badala ya mchoro mmoja kupita juu au ndani ya mwingine basi waruhusu wafanye hivyo.
Kumbuka kuwa sababu na maelezo yanayotolewa ni muhimu kuliko mchoro wenyewe.

10. Mlinganisho (Ranking)

Mjadala kuhusu matatizo, fursa, na fursa zilizopo katika myanja mbalimbali maendeleo katika jamii pia itahusha makundi mbalimbali ndani na nje ya jamii hiyo ambayo yanahusika kwa kwa namna mbalimbali.

Mjadala huu ni lazima utazungumzia umuhimu wa kulinganisha vipengele mbalimbali vya suala lile linalozungumziwa kama sehemu ya mchakato wa kulichunguza ili kulielewa na kuweza kulifanyia uamuzi mzuri.

Ili kuweza kulinganisha na kuamua ni kipi kina umuhinu mkubwa zaidi, sharti uanze kwa kuviorodhesha namna ambayo itaonesha tofauti zilizipo kati ya vitu hivyo. Ni vizuri kwa mfano kubaininsha ama matatizo au matakwa ya washiriki na kuangalia ni vigezo gani vya kutumia katika kuweka vitu hivyo katika mpangilio fulani. Hii inawezesha pia vipaumbele vilivyotolewa na vikundi tofauti kulinganishwa

Utoaji wa alama (ranking) kwa orodha ya masuala yaliyobainishwa inaweza ikatumika ama kwenye usaili (ikasaidia kupata maelezo ya kina kwenye SSD) Inaweza pia ikatumika peke yake. Mlinganisho unaweza pia ukatumika katika kukusanya habari nyeti kama vile mapato, na uwezo wa mtu .kv. idadi ya mifugo.

Ingawaje kuna aina mbalimbali za mlinganisho ambazo zinatumika zaidi ni hizi zifuatazo;

- ***Preference Ranking:*** ambayo watu wanapiga kura kura kufanya uchaguzi wa kipi kimoja wanakipendelea.,

- ***Mlinganisho wa jozi :*** ambayo imbapo choro unatengenezwa wa kusaidia kufanya mafananisho wa vitu viwili viwili.

- ***Direct matrix ranking*** **:**Hii inasaidia kwanza kwa washiriki kutengeneza vigezo vitakavyotimika kwa kufanya uchaguzi. Hii inatumika hasa pale ambapo unataka kuelewa sababu za kuchagua vitu kama mbegu fulani ya mifugo,mahindi, mhogo n.k Vigezo maa nyingi vinaweza kubadilika kutoka kikundi kimoja hadi kingine kwa mfano vigezo vinavyotumika

- ***Mlinganisho wa uwezo wa kaya***: Ambapo wanajamii wanajigawa katika makundi kadhaa kufuatana na uwezo ambao kila mmoja anao. Wakitoa sababu walizotumia kuwagawanya katika makundi, kutoa maelezo ya jinsi gani watu wanitumbia au kujnasua na haoc makundi

- ***Mlinganisho wa wadau (Stakeholder ranking):*** Hii inachunguza maoni ya Kuchunguza maoni ya washiriki kuhusu mahusiano baina ya mradi na wadau mbalimbali (*taasisi za serikali, makundi ya watu, taasisi zisizo za kiserikali, wafanyi biashara n.k.)*

11. Mlinganisho (Simple)

Madhumuni

- Kupata maoni ya washiriki kuhuhusu wanayopenda na wasiyopenda
- Kupata maoni ya washiriki kuhusu suala fulani kwa kuchambua namna mbalimbali wanazoweza kutumia kukabili.
- Kuchunguza sababu ambazo zinafanya washiriki wachague vitu mbalimbali wanavyopendelea.

Mbinu

- Elezea suala unalotaka lizungumziwe.
- Washiriki wachangie kwa kueleza namna mbalimbali zinazoweza kutumika kutatua suala hilo. Orodhesha njia mbalimbali zinazoelezewa na washiriki kwenye karatasi.

- Ziweke njia hizo zilizoelezewa kwenye makundi kadhaa na ndipo utakapoweza kuzipima kwa uzito ipi ya juu na ipi ya chini. Bainisha kundi liloko juu zaidi kwa uzuri au kwa udhaifu. Waruhusu washiriki kuchagua maneno ambayo kwao yanaelezea vigezo vizuri zaidi.

  Mfano: Katika kusema aina ya ngombe anayependwa zaidi na asiyependwa sana, washiriki wenyewe watapitia na kutoa sifa/ vigezo hadi watakaporidhika na sifa za aina ya ngombe anayependwa zaidi na yule asiyependwa.

  Katika kupima na kutoa sifa za maeneo mbalimbali za Ngorongoro washiriki waligundua kuwa waliishia kuwa na sifa nyingi sana kuhusu maeneo mazuri zaidi na yale ambayo siyo mazuri. Pengine wangekamilisha zoezi hili mapema kama wangechagua ni “eneo gani la Ngorongoro ambalo wangependa kuishi”.

- Waeleze washiriki kuwa wanatakiwa kuorodhesha uchaguzi wao kwa kuanzia kile kijiji ambacho wanakipenda zaidi, ikiendelea kupungua kwa sifa hadi waishie na kijiji ambacho hawakipendi kabisa. Upande mmoja wa ukurasa uitwe eneo zuri zaidi na upande mwingine uitwe eneo lisilopendwa kabisa.

- Eleza pia kwamba washiriki wanaweza kuwa na makundi mengi kwa kadri inavyohitajika, k.m vijiji vitatu kwenye kila kundi la;vizuri sana, vizuri, wastani, mbaya, mbaya sana.

- Wasaidie washiriki kwa kupendekeza waanze na kuchagua ama vijiji vilivyo vizuri kabisa au vile vilivyo vibaya sana.

- Wasikilize kwa makini sababu wanazotoa katika kufanya uchaguzi wa vijiji.

- Baada ya kukamilisha zoezi ka kupanga vijiji kufuatana na kipi kinapendwa zaidi, uliza ni vipi sifa za kijiji kimoja ambacho si kizuri zinatakiwa zibadilike ili iweze kubadilisha nafasi yake na kuwa kizuri. Vile vile, ni vipi kijiji ambacho kina sifa ya kuwa kuzuri kinaweza kubadilisha nafasi yake kutoka kuwa kizuri na kuwa kibaya.

Katika kufanya zoezi hili, lengo lako kubwa siyo kijiji kipi kinaishia kuwa kwenye nafasi ipi ila ni sababu zipi na vigezo vipi vinatumika kwa kufanya uamuzi. Hii itarahisisha mjadala wa vitu gani vinafanya kijiji kiwe kizuri au kibaya kufuatana maoni ya washiriki.

Kama mnachozungumzia ni ipi minada mizuri zaidi ya kununulia ng'ombe, unategemea kupata vigezo mbalimbali na uzito/ umuhimu wa hivyo vigezo utachangia katika uchaguzi wa minada ipi mizuri zaidi. Zoezi hili kwa mfano litaonyesha kama kwa mfano ukaribu ni kigezo muhimu zaidi au bei inayotolewa, au ubora wa ngombe inayoletwa.

Mfano mlinganisho wa baadhi ya minada

	Endulen	Olbalbal	Kakesio	Mbulu	Matepes
Bei nzuri ya kununulia					
Mnada una uzio mzuri na usalama					
Kuna ulinzi mzuri					
Bidhaa nyingi za nyumbani kwa bei nzuri.					
Dawa za mifugo zinauzwa kwa bei nzuri					
Siyo mbali sana					
Usalama mkubwa njiani					
Kodi na usumbufu wa malipo ni mzuri					
Kuna mizani ya kupima uzito wa mifugo					
Wanunuzi wa kutoka mbali wanafika					
Vyakula na vinywaji vinapatikana kwa wingi na bei nzuri					
Alama					

Alama 1 = chini sana
5 = juu sana

12. Mlinganisho wa jozi - *Pairwise Ranking,*

Madhumuni:
Mbinu hii inatumika kuchunguza kwa makini zaidi misingi ya washiriki wanayotumia katika kufanya maamuzi fulani. Kwa mfano ni tatizo gani kubwa zaidi, au ni kipi wanachokipendelea

Jinsi ya kutumia mlinganisho wa jozi:

Ingawaje mbinu hii inaweza kutumika kuchunguza matatizo, na uwezekano wa kuyatatua, mara nyingi hutumika kubainisha yale ambayo yanapendwa na yasiyopendwa. Ni mbinu nzuri vilevile ya kulinganisha vitu vinavyofanana kama vile aina ya vyakula, aina/ mbegu za mifugo, nk. Hata hivyo inawezekana pia kulinganisha vitu vilivyo tofauti kabisa na unapoanza zoezi hili huwezi kufahamu kama washiriki wanaona tofauti yeyote kati ya vitu hivi.

Kwa mara ya kwanza utakapofanya zoezi hili, kuna uwezekano mkubwa kwamba itakuchanganya na utakosea. Anza kwa kuelezea vitu vinavyolinganishwa katika upande mmoja. Kama hujui ni jumla ya vitu vingapi vinavyolinganishwa ni vigumu kufahamu uache nafasi kubwa kiasi gani ya kujaza kwenye karatasi.

Njia rahisi ni ya kuhakikisha kuwa sehemu zote za mchoro zilizoorodheshwa zinapitiwa ni kuweka idadi ya vitu vilivyoorodheshwa katika pande zote mbili za mchoro. Anza kwa kuweka alama ya "***x***" pale ambapo kitu kimoja kinafananishwa na chenyewe katika misitari ya pande zote mbili. Endelea kwa kufanyia kazi upande mmoja wa mchoro mraba na uwaulize washiriki kuhusu uchaguzi wao kati ya vitu viwili viwili vinavyofananishwa.

Kwenye mchoro ulioonyeshwa hapo chini, unaweza ukaamua kufanyia kazi sehemu ya juu ya mchoro na ukaanza kwa kufananisha namba 1 na namba 2 halafu endelea kwa kulinganisha namba 1 na namba 3 na halafu 1 na 4. Endelea kwa kuwauliza washiriki wafananishe 2 na 3, na halafu 2 na 4 . Katika kufananisha washiriki wanaambiwa wachague moja kati ya vitu viwili vinavyokinganishwa na uchaguzi wao ndio inaoingizwa katika kisanduku husika katika mchoro.

	1	2	3	4
1	x			
2		x		
3			x	
4				x

	1	2	3	4
1	x			
2		x		
3			x	
4				x

Kama unalinganisha vitu vinne unahitaji kufananisha vitu viwili viwili mara sita.

Na kama unao muda wa kutosha, unaweza ukaandaa mchoro ambao utarahisisha mlinganisho kwa kuwa utaepuka kurudia rudia na utakuwa rahisi kutumia. Hii itawezekana ikiwa utaruka kitu cha mwisho kwenye upande mmoja wa mchoro na cha kwanza kwenye upande mwingine wa mchoro na bado utakuwa na mchoro utakaokuwezesha kufanya mlinganisho wa vitu viwili viwili mara sita.

	1	2	3
2			

3			
4			

Ukifikia mwisho wa mlinganisho wa jozi, mchoro wako utakuwa na na matokeo ya uchaguzi mbalimbali uliofanyika ambao unaweza ukawasilisha kwa washiriki kama ndicho walichagua kuwa wanapenda.

Majadiliano wakati wa kufanya uchaguzi baina ya vitu viwili viwili na mwishoni wakati wa kufanya majumuisho ya matokeo ni muhimu zaidi kuliko uchaguzi wenyewe. Inawezekana ikatokea kuwa washiriki wasikubaliane na kile kilichojitokeza kama ndio chaguo lao. Hii mara nyingine hutokea kutokana na sifa muhimu zaidi ambayo inaathiri uchaguzi kuliko nyingine.

Mlinganisho jozi kwa kijiji cha Kakesio

	Maji ya matumizi ya nyumbani	**Maji ya kunyweshea mifugo**	**Afya ya mifugo**	**Afya ya binadamu**	**Elimu**	**Kilimo**
Maji ya matumizi ya nyumbani		Maji ya matumizi ya nyumbani	Maji ya matumizi ya nyumbani	Maji ya matumizi ya nyumbani	Maji ya matumizi ya nyumbani	Maji ya matumizi ya nyumbani
Maji ya kunyweshea mifugo			Afya ya mifugo	Afya ya binadamu	Elimu	Kilimo
Afya ya mifugo				Afya ya binadamu	Elimu	Kilimo
Afya ya binadamu					Afya ya binadamu	Afya ya binadamu
Elimu						Elimu
Kilimo						

13. Mlinganisho sababishi (Matrix ranking)

Madhununi:

Hii inasaidia kufuatilia kwa kina zaidi ili kupata kujua maoni na sababu za washiriki kufanya uchaguzi unaoonesha kupendelea vitu fulani badala ya vingine.

Kuchunguza ili kuelewa tofauti za washiriki kimawazo kuhusu masuala mbalimbali kama yanavyojionyesha kwa kupitia sababu zinazowafanya wapende au wachague vitu fulani na kutokupenda vingine.

Kubainisha na kujadili kwa pamoja mawazo na hisia zinazowafanya watu waamue kuchagua kitu kimoja na siyo kingine.

Mbinu
Tengeneza orodha ya vitu ambavyo vitahitaji kujadiliwa na vigezo vitakavyotumika katika kuvijadili na kuvipa alama ya kuonyesha ni kwa kiasi gani kila kimoja kinapendwa na hatimaye kupewa uzito au kipaumbele kufuatana na alama ambazo kila mmoja imezipata.

- k.v aina mbalimbali za ngombe, na kwa kila aina
- kujadili vigezo kama vile; utoaji wa maziwa, ukubwa/ uzito, muda anaochukua ili kuweza kuzaa, muda anaochukua ili kuweza kuuzwa kwa bei nzuri, uwezo wa kustahimili magongwa, mvuto (pembe, nundu),

Jadili vigezo vinavyotumika: kuamua ni nini kizuri au kibaya kuhusu kitu hicho.

Majadiliano kuhusu kitu cha kwanza kinachojadiliwa yafanyike taratibu, ili kuwapa washiriki nafasi ya kuielewa vizuri. Hii pia itaruhusu vigezo vingine vinavyoweza kutumika kujitokeza taratibu.

Wahakikishie washiriki kuwa wanaweza kuongeza vigezo vingine.

Kama ikibidi pendekeze vigezo uwe wazi kuwa hiyo imependekeza wewe na siyo wao.

Anza kuchora na uache nafasi ya kutosha kupanua mchoro kwa kuongeza vigezo vingine.

Pima uzito wa kila kimoja kufuatana na hoja na washiriki wanaoipendelea na kutoa kipama umbele kama idadi ya vitu vinavyojadiliwa ni fupi (*vitu hadi kumi vinawezekana kuwekea uzito na kipaumbele, ila vikizidi inakuwa ngumu zaidi).*

Jaribu kutumia vitu ambavyo ni rahisi kuhesabu kama vile mbegu, kokoto/mawe, mavi ya mbuzi, vijiti vikavu au vibichi, nk. katika kutoa alama kwa kuwa ni rahisi kuzibadilisha pale inapohitajika ama kupunguza au kuongeza na pia ni rahisi kwa washiriki wote hata wasiojua kusoma kushiriki.

Vigezo viwekwe kwa namna ambayo ni chanya
Hakikisha kuwa utaratibu wa kutoa alama ni unatumika kwa vitu na vigezo vyote; kwa mfano alama za chini (1, 2,) zionyeshe hali nzuri na alama za juu (5, 4,) zionyeshe hali mbaya, au

kinyume chake. Ni muhimu utaratibu mmoja utumike pasipo kubadilika badilika. Unaweza ukahitaji kubadilisha vigezo vya hali chanya kuwa hasi.

Tafuta mifano ya kitu chenye alama za juu, kuonyesha kuwa kitu hicho kinapendwa, au kuchukiwa. Vilevile tafuta vitu vyenye alama ambazo si za kawaida kwa mfano pale ambapo kwa kigezo kimoja inatolewa alama ya juu na kwa kigezo kingine inatolewa alama ya chini sana.

Usijaribu kujumlisha jumla alama kwa zilizopatikana kwa kila kigezo. Tazama pale palipo na alama za juu au alama za chini na utafute sababu zake kwa kuulizia.

Uliza washiriki wachague kitu kimmoja tu wanachokipenda, na uwaulize ni kwa nini wanakichagua hicho.

Maelezo washiriki wanayotoa ni muhimu zaidi kuliko mchoro wenyewe.

Mlinganisho wa matrix

	Maharage	**Dengu**	**Njegere**	**Kunde**
Vigezo				
Inazaa kwa wingi	4	3	2	1
Inastahimili wadudu waharibifu	3	3	4	2
Mahitaji ya matunzo/ au kazi ni madogodogo	2	4	1	3
Mapishi yanachukua muda mfupi kuni kidogo.	1	4	2	3
Ladha nzuri	1	2	3	4
Hayasabisha gesi ya tumboni na kuvimbiwa	1	4	3	2
Majani yake yanafaa kwa mboga za majani	1	2	3	4
Yanastahimili ukame	2	3	1	2
Bei nzuri ya mauzo	2	4	3	1

14. Mlinganisho wa hali ya maisha ya kaya (Well Being Ranking)

Madhumuni

- Kuelewa maoni ya washiriki kuhusu hali nzuri ya maisha
- Kubainisha vigezo vinavyotumika na jamii kwa maisha mazuri
- Kujua nafasi ya kaya mbalimbali katika jamii kufuatana na vigezo vilivyowekwa.

Mbinu

Tengeneza orodha ya kaya zote zilizopo hapo kijijini kwenye kadi au karatasi.

> Hii inaweza ikafanyika kwa kutumia njia mbili . Ya kwanza ni kwa kuwambia washiriki wakumbuke majina ya kaya zote kijijini. Inaweza kuwa ni vizuri kutengeneza orodha mbili, moja ya wanaume na ingine ya wanawake pale inapoonekana kuwa walio na hali nzuri na wale wenye hali mbaya wanaishi pamoja (k.v. mume ana hali nzuri na mke ana hali mbaya).

Uwe tayari kugawanya wanakijiji katika sehemu mbili au zaidi ikiwa washiriki wanaielewa vizuri sehemu na ingine hawaielewi vizuri.

Andika jina la kila kaya kutoka kwenye orodha kubwa kwenye kipande cha karatasi ndogo au kadi ndogo. Itakuwa ni vizuri kuipa kila kadi namba yake.

Baadhi ya washiriki ambao wameishi kwa muda mrefu zaidi katika kijiji wachaguliwe kusailiwa kuhusu hali ya kaya. Usaili ufanyike na kikundi cha wanaume peke yao na wanawake pia peke yao. Uliza kama wasailiwa kama wanataka wanaume na wanawake wachambuliwe tofauti au kwa pamoja.

Mwambie kila msailiwa achambue kadi na kuziweka katika makundi kufuatana na hali ya kaya hiyo kuwa ama nzuri au mbaya. Wanaweza kuwa na makundi mengi kadri inavyohitajika na makaratasi ya kila kundi yawe na boksi au kikapu kidogo. Upande mmoja uwa na kadi za wale wenye hali mbaya na upande mwingine uwe na kadi za wale wenye hali nzuri.

> Anza kwa kumpa msailiwa kadi mmoja moja huku ukiisoma ikiwa msailiwa hajui kusoma. Kadi ya pili inaweza kuwekwa ama chini au juu ya ile ya kwanza kufuatana na uamuzi wa msailiwa.
>
> Endelea kumpatia msailiwa kadi nyingine na umwambiwe aziweke katika makundi husika. Wawe huru kuunda makundi mapya endapo kadi haiingii vizuri katika makundi yaliyopo.
>
> Msailiwa anaruhusiwa kuweka kadi pembeni iwapo anaona kuwa haielewi kaya hiyo vizuri. Msailiwa asiiweke kadi yake kwenye makundi.
>
> Endelea hadi kadi zote zimewekwa kwenye mojawapo kati ya makundi.

Chukua kila kundi la kadi na usome majina ya kaya zilizopo kwenye kundi hilo. Muulize msailiwa kama anaridhika na majina hayo kuwa kwenye kundi hilo na kama haridhiki abadilishe. Muulize msailiwa ni sifa ipi inayozifanya kaya hizo ziwe kwenye kundi hilo. Sababu zitakazotolewa ndizo vigezo vya kuonyesha hali nzuri na hali mbaya.

Endelea kufanya hivi kwa kila kikundi.

Uliza vingine vya hali nzuri au mbaya kwa kuuliza ni vipi kaya moja inaweza kutoka kwenye kundi moja na kwenda kwenye kundi lingine. Kaya zilizopo kwenye kundi la chini zinawezaje kupanda kwenda kwenye hali nzuri na zilizopo kwenye hali nzuri zinawezaje kushuka kuja kwenye hali mbaya.

Kila kadi iwekewe alama kwa nyuma inayoonyesha kundi ambayo imewekwa. Endapo msailiwa ameziweka kwenye makundi matano, kadi zilizopo kwenye kundi la tano ziandikwe 1/5; zilizopo kundi la pili ziandikwe 2/5; zilizopo kwenye kundi la chini kabisa ziandikwe 5/5. Kama msailiwa mwingine ameziweka kwenye makundi sita, alama zitakazoandikwa nyuma ya kadi zitakuwa 1/6, 2/6, nk hadi kufikia 6/6.

Tazama kama kuna kaya ambazo kuna tofauti kubwa kati ya alama iliyotolewa na wasailiwa, k.v mmoja ameipa alama ya chini sana wengine waipa alama ya juu sana.

Pale ambapo wasaili wote wametoa alama ambazo karibu zinafanana , hii inadhihirisha kuwa alama hizo zinathibitisha usahihi wa maoni ya washiriki kuhusu hali nzuri na hali mbaya.

Jumlisha alama za kila msailiwa upate upate wastani wa alama kwa kila kaya.

Zipange kaya zote kufuatana na alama ambazo imepewa. Hii itatoa sura ya nafasi ya kila kaya kufuatana na kama ina hali nzuri au mbaya.

Mfano wa Ankara ya hali nzuri						
Namba ya kaya	Msailiwa				Wastani wa alama	makundi
	A	B	C	D		
39	20	20	11	25	19	Hali nzuri
33	20	20	11	25	19	
14	20	20	22	25	21	a
40	20	20	22	25	21	
16	20	40	22	25	26	
12	20	20	44	25	27	
18	20	40	33	25	29	b
28	20	40	33	25	29	
24	40			25	32	
41	20			50	35	
21	20	40	56	25	35	
46	20	40	56	25	35	
42	20	40	44	50	38	
30	20	60	56	25	40	c
8	20	40	56	50	41	
9	20	40	56	50	41	
37	40	40		50	43	
31	40			50	45	
22	20	60	56	50	46	
15	40	40	56	50	46	
27	20	60	56	50	46	
17	20	60	67	50	49	
23	40	60	56	50	51	
36	40	60	56	50	51	
47	40	60	67	50	54	
11	40	60	67	50	54	d
20	40	80	67	50	59	
4	40	60	67	75	60	
43	40	60	67	75	60	
6	40	60	67	75	60	
38	20		67	100	62	
19	40	60	78	75	63	
32	40	60	89	75	66	
35	60			75	67	
25	40	80	89	75	71	
10	40		78	100	72	e
7	60	80	89	75	76	
45	80	40	100	100	80	
48	60	80	89	100	82	
44		80	67	100	82	
5	60	100	89	100	87	
2	60	100	89	100	87	
13	80	80	100	100	90	
3	60	100	100	100	90	f
34	60	100	100	100	90	
26	80	80	100	100	90	
1	80	100	89	100	92	
29	100	100	100	100	100	Hali mbaya
Jumla ya Makundi	5	5	9	4	5	

Sifa na vigezo vya kaya yenye hali nzuri ya maisha

	Ngutot	Osinoni	Esere
Kaya yenye hali nzuri ya maisha	• Jitihada kubwa ya kazi • Wafanya biashara wa mifugo • Vijana wameajiriwa kwa ulinzi mikoa ya Shinyanga na Mwanza. • Wameoa wake wachache (1-2) • Wamepata msaada wa Ewoloto • Wanatumia madawa kutibu mifugo • Wanauza asali	• Wanatumia madawa kutibu mifugo • Wanalima • Ewoloto • Wana watoto wa kuwasaidia • Wana umoja • Wamepewa mifugo na wazazi wao • Vijana wanafanya kazi Shinyanga	• Ana mume anayemtunza na mume wake ni kijana • Anao wamorani ambao wanamtunza • Ana mifugo ya kutosha • Ana ngonbe kiasi na ni tajiri • Morani wake ni wafanyi biashara wa ngombe • Amesaidiwa na Mradi wa Ereto pamoja na ndugu zake. • Ndiye mke wa kwanza hivyo an mifugo mingi. • Ingawaje ana ngombe wengi amewekwa nafasi ya chini kutokana na kuya na watoto wengi. • Ingawaje amepewa mifugo na Mradi wa Ereto amewekwa kwenye nafasi ya chini kwa sababu hana mume.
Kaya yenye hali duni ya maisha	• Mume amefariki • Watoto ni wadogo • Mifugo kuibiwa • Magonjwa ya mifugo • Alipewa mifugo michache wakati alipoolewa • Ndoa ya mitara • Kwa sababu ya kuzaa watato wengi.	• Kuwa na familia kubwa • Kutokuwa na mifugo • Kutopatiwa msaada wa Ewoloto • Hawana watoto wa kuwasaidia • Watoto wamekua .	• Hamna mifugo • Hana mume wa kumtunza • Mume ana wake wengi lakini mifugo ni michache • Ngombe walikufa kutokana na magonjwa. • Aliolewa mke wa mwisho na mumewa wakati ambapo mifugo ilipewa mke wa kwanza na wa pili. • Mume na mke wamezeeka na wanaye kijana mmoja tu ambaye bado ni mdogo.

15. Wadau - Stake holder Ranking

Madhumuni:
Kuchunguza maoni ya washiriki kuhusu mahusiano baina ya mradi na wadau mbalimbali (*taasisi za serikali, makundi ya watu, taasisi zisizo za kiserikali, wafanyi biashara n.k.)*
Kufanya zoezi ambalo litaruhusu kuuliza maswali kuhusu wahusika wakubwa katika mradi *(e.g. Wahisani, Serikali kuu, Halmashauri ya Wilaya, Bodi, Wafanyikazi wa Mradi,)* na kuna mahusiano gani kati yao.

Mbinu
Muda saa 1
Vifaa vitakavyotumika: Karatasi kubwa la Filipchart, Kalamu kubwa –markers, Vikaratazi vidogo kama kadi, masking tape, n.k

Elezea kuwa madhumuni ni kutazama mahusiano bain ya mradi na wadau au makundi mbalimbali ya watu na mashirika yanayohusika na mradi.

Tazama maana ya neno "mdau, wadau". Wote wale ambao mradi unawagusa kwa namna moja ua ingine. Pengine mradi unawanufaisha binafsi kama vile kutatua matatizo yanayowakera, au unaendeleza agenda au masuala ambayo wanaona ni muhimu na ambayo huwa wanayasukuma kwa namna mbalimbali. Hata wale ambao mradi unaathiri maslahi yao kwa namna moja au ingine pia ni wadau.

> *"Mtu binafsi, kundi, taasisi au shirika ambalo linastahili kupata sehemu ya raslimali ya mradi ikiwa ni pamoja na muda, au linaweza likashawishi mradi ufanye nini au ambao kwa namna moja au ingine wanaathirika na matokeo ya kazi mradi unaofanya*".

Eleza kuwa maana yake ni pana na kuwa lengo ni kutoa nafasi kwa washiriki waweze kubainisha wadau wengi kwa kadiri inavyowezekana.

Washiriki wafikirie na kusema majina ya wadau wa mradi kama wanavyoona huku ukiyaandika. Katika hatua hii nia ni washiriki wataje majina yote bila kuyajadili. Elezea kuwa baadaye kutakuwa na nafasi ya kujadili, kuongeza na hata kuzipunguza.

Vikaratasi vyenye majina ya wadau yanayotajwa yabandikwe kwenye Flip chart.

Kama washiriki ni wengi wagawanyike kwenye makundi mawili na kila kundi lijadili wadau waliopendekezwa na kuwapanga kwa kipaumbele kuanzia na wale walio na sauti kubwa zaidi katika mradi na wale wanye sauti ndogo kabisa waje chini/nwisho. Upande wa juu wa Flipchart uuandikwe "*wenye sauti zaidi*", na upande wa chini uandikwe "*wenye sauti ndogo zaidi*". Mtu mmoja awe anaandika hoja zilizotolewa na washiriki hasa pale ambapo mdau mmoja anaonekana kuwa na sauti kubwa zaidi kuliko wengine.

Vikundi vikutane na kujadili hoja zilitumika na kila kimoja katika kupanga wadau katika nafasi mbalimbali za umuhimu.

Eleza kwamba zoezi hili linapaswa kuangalia hali halisi ilivyo katika mradi kwa sasa na siyo hali wanayotaka iwe baadaye. Makundi mabalimbali yanaweza kujitokeza k.v. (wenye sauti kubwa, wenye sauti ndogo) n.k.

Ni muhimu kupata ni sababu zipi zinafonya kundi moja kuwa na nguvu kuliko lingine. Angalia kama sababu zote zilizotolewa ni sawa na kama kuna ambayo imesahauliwa.

Uliza washiriki kama wana maswali yeyote au kitu wanachohitaji kielezewe zaidi kuhusu zoezi hilo.

Nakili orodha ya wadau kama ilivoandikwa kufuatana na umuhimu. Unaweza pia ukaandika namba ambayo kila mdau amepewa nyuma ya kadi yenye jina la mhusika.

Waelekeze washiriki wafanye tena zoezi hilo kwa kuzingatia wale ambao wangependa zaidi kuwaridhisha na wale ambao hawawajali sana bila kujali kama wana sauti zaidi au siyo.

Washiriki watazame na kujadili tofauti kati ya orodha hii na ile orodha ya kwanza.

Kupanga wadau huria. (***Free mapping***)

Badala ya kuwapanga wadau katika msitari kwa kuanzia na walio na sauti zaidi, tumia mchoro ambao mradi unakuwa katikati ya karatasi na wadau wapangwa kwa kuuzunguka mradi. Wadau walio na sauti zaidi wanakuwa karibu zaidi na mradi na wale wasio na sauti mbali zaidi wakifuatiwa na wale wenye sauti ndogo. Mbinu inatoa nafasi kwa washiriki kuonesha vizuri zaidi masuala yanayohusu mahusiano ya mradi na wadau. Hii ni kwa kuwa wanaweza kuweka wadau karibu au mbali na mradi kwa kuonesha sauti na uwezo, na wanaweza vilevile kuweka mistari yenye unene tofauti ili kuonesha mambo memgine katika mahusiano kama vile, umuhimu, ukubwa wa misaada ya hali na mali wanayotoa n.k.

Kupanga Wadau kwa umuhimu kwa kutumia vigezo viwili

Badala ya kuwapanga wadau kufuatana kwanza na umuhimu halafu baadaye kuwapanga tena kufuatana na sauti waliyo nayo washiriki wanaweza wakatumia vigezo vyote viwili kwa wakati mmoja. Utahitaji kuwa na karatasi lenye nafasi ya kutosha ili kuweka vigezo vyote viwili kila kimoja kikiwa na sehemu yake.

	Umuhimu mdogo	***Umuhimu mkubwa***
Sauti ndogo katika Maamuzi		Walengwa
Uwezo mkubwa	Wahisani	

Mfano mzuri ni wadau wanaopshana sana ni wahisani ambao wana uwezo mkubwa wa kifedha, na alengwa ambao ni muhimu sana kwa mradi lakini hawana uwezo mkubwa.

16. Chimbuko la matatizo (Mchoro wa vyanzo na athari)

Madhumuni

Kuchunguza na kujadili kuhusu vyanzo vya matatizo yanayojitokeza.

Kubadilishana mawazo kuhusu yale yanayosababisha matatizo.

Kujadili njia mbalimbali zinazoweza kutumika kutatua matatizo

Baada ya usaili kubainisha tatizo:

Andika tatizo kwa kifupi na uanze kuchunguza vinavyosababisha tatizo.
(*ingawaje linaweza lisiwe ndilo tatizo la msingi, linachukukuliwa kama mahali pazuri pa kuanza)*

Uliza ni nini kimesababisha tatizo.
Chunguza vyanzo na sababu mbalimbali za tatizo.

Chunguza kila sababu upate kujua washiriki wanafikiri ni nini kinachangia katika sababu hizo zilizotajwa. Hii itasaidia kupata *mizizi ya tatizo* na hatimaye kubainisha *tatizo la msingi* au *kiini cha tatizo* ni nini.

Uliza ni kwa nini hali iko hivyo, nini kinasababisha, nini kingine kinachangia katika kusababisha hali hiyo.

Wakati unachunguza mizizi ya tatizo epuka kuuliza “kwa nini hili ni tatizo” kwa kuwa majibu ya swali hili yatakuelekeza upande mwingine wa mti usiotakiwa kwenda yaani kule juu ulikotoka.

Pale ambapo tatizo majadiliano yanaelekea kukwama (k.v hakuna fedha) endelea na kuchunguza visababishi vingine.

Wasaidie washiriki kujadili matokeo/ athari za tatizo.

Chunguza na kupata maoni ya washiriki kuhusu matokeo na athari za tatizo.

Katika sehemu ya kwanza ya majadiliano mkazo uwe ni kwenye sababu za tatizo na athari ambazo kimsingi zinaonyesha hali mbaya.

Chunguza ni sababu zipi zinazoweza kutatuliwa na zipi zipo nje ya uwezo wa washiriki kutatua.

Ikiwa mti huu umefanyiwa kazi vizuri kama ukiugeuza matatizo kuwa ufumbuzi, mchoro huo bado utakuwa umekaa vizuri kama mti wa ufumbuzi.

Majadiliano pia yanaweza yakatazama jinsi sababu hizo zinavyoweza kugeuzwa kuwa ni hali nzuri ambapo tatizo litakuwa limeshatatuliwa.

Kumbuka kwamba sababu zinazotolewa wakati wa majadiliano ni muhimu zaidi kuliko majibu yenyewe.

Kampuni ya kuuza madawa



17. Utatuzi wa matatizo

Madhumuni

- Kutazama uwezekano wa kupata ufumbuzi wa matatizo mbalimbali yaliyobainishwa kwenye mti wa matatizo.
- Kutengeneza orodha ya namna ambavyo matatizo mbalimbali yanaweza kutatuliwa.
- Kujadili yale yanayowezekana kufanya na yasiyowezekana kufanyika katika hali mbalimbali.

Mbinu (jinsi ya kutengeneza)

Mti wa ufumbuzi wa matatizo unakuwa tu na maana pale ambapo zoezi hili linaendelea kukamilisha kulichofanyika kwenye mti wa matatizo.

Utaratibu wa kutumia ni rahisi ila unahitaji uangalifu mkubwa.

Matatizo yote na vyanzo vyake yaliyobainishwa kwenye mti wa matatizo yaandikwe kuonyesha ukosefu au hali mbaya. Ili kutengeneza mti wa utatuzi ni muhimu haya yote yageuzwe kuwa katika hali nzuri.

Ni muhimu kuwa makini na mwangalifu kwani kazi kubwa ni kubadili kila kilichoandikwa kutoka hali nzuri kuwa mbaya.

> Kwa mfano: Tatizo linaweza kuwa ni "*kutokufahamu mahitaji ya wafugaji ya dawa za kinga na tiba kwa mifugo kwa misimu mbalimbali*" na "*kujua vizuri mahitaji ya wafugaji ya dawa za kinga na tiba kwa misimu mbalimbali"*.

Kumbuka kwamba ni rahisi kuanza kuandika majibu yanayozekana kwa kila jawabu bila kuangalia kwa makini kama hayo ndiyo peke yake majibu sahihi au yanayowezekana kwa tatizo hilo.

Inawezekana kukawa na matatizo ambayo kampuni haitaweza kuya shughulikia.
kwa mfano; Dawa ya tiba kwa magonjwa mengine bado haijagunduliwa. Inaweza ikawa wanaweza kushauri tu, au kusaidia kuwekea nguvu hoja ya serikali kuimarisha utafiti kuhusu magonjwa sugu ya mifugo ambayo hayan a tiba wala kinga.


Kampuni ya kuuza madawa
Mapato mazuri
Mauzo mengi
Wateja wapata huduma za kuridhisha
Magonjwa mengine ya mifugo bado haijapata tiba
Dawa zinazohitajika kwa milipuko ya magonjwa zinapatikana
Dawa hazijapita muda wake wa matumizi
Ushauri mzuri unatolewa kuhusu matumizi ya dawa kwa tiba na kinga
Mtaji wa kutosha
Ufahamu mkubwa kuhusu mahitaji ya dawa za tiba na kinga.
Uagizaji na ununuzi wa dawa unasimamiwa vizuri
Ushauri mzuri unatolewa kuhusu kinga na matumizi ya dawa.
Uwezo mzuri wa kusimamia mtaji na kutafuta nyongeza
Uwezo mzuri wa kusimamia na kuendesha biashara
Wana uwezo wa kuhudumia wateja vizuri.
Wahudumu wanajua matumizi ya dawa
Uwezo mzuri wa kusimamia na kuendesha biashara ya dawa za mifugo.

18. Mchoro Unaobainisha uwajibikaji ni lini

Madhumuni:
Kusaidia kuchagua katika yale yanayowezekana li kuleta mabadiliko.
Kuangalia ni nini kinawezekana kufanyika na kufanya mipango mizuri.

Zoezi hili linakuwa na maana zaidi hasa pale ambapo washiriki wameshatafakari namna mbalimbali ya kutatua tatizo hasa baada ya kuangalia mti wa ufumbuzi wa matatizo. Kwa kuwa zoezi hili linasaidia kutoa vipaumbele na kuchuja ni vizuri kuruhusu mazoezi mengine kutoa uwezekano mbinu mbalimbali za utatuzi hata kama njia nyingine zinaonekana ni za ajabu.

Mbinu

Njia mbalimbali zinazopendekezwa kama utatuzi ziandikwe au zichorwe kwa kutumia karatasi ambalo linaweza kuwekwa ukutani na kubanduliwa.

Ingawaje njia nyingine za utatuzi zinaweza zikaendelea kupendekezwa hii itawavuta washiriki nje ya zoezi la kuweka kipaumbele ambalo litakuwa linaendelea.

Kama una njia nyingi za utatuzi zilizopendekezwa na unajaribu kuziorodhesha kufuatana na umuhimu, itakuwa ni vizuri kuchagua chache ambazo zitapewa kipaumbele na hizo ndizo zifanyiwe kazi.

Uwe na nafasi kubwa ambayo njia mbalimbali zilizopendekezwa zinaweza kubandikwa na hata kutolewa na kusogezwa kufuatana na nafasi itakayopewa katika umuhimu.

Vigezo vya umuhimu vinaweza vikawa ni *sasa, mapema,* au *baadaye* vikae katika upande mmoja na upande mwingine kuwe na; haina manufaa, ina manufaa kiasi, ina manufaa zaidi.

	Sasa hivi	Baada ya muda mfupi	Baadaye
Msaada hauhitajiki	xxx		
Msaada kiasi unahitajika		xxxxxxx	
Msaada mkubwa unahitajika			xxxxxxxxx

Zile njia za utatuzi ambazo zitakuwa zimewekwa katika sanduku la juu kushoto ndizo zinazoweza kuanza mara moja na baadhi zinaweza kuanza mara moja kwa ajili ya kupata uzoefu na kama manufaa ya kushiriki katika zoezi hili .

Yale mawazo ambayo yamewekwa kwenye sanduku la chini, yanahitaji pia yafanyiwe utambuzi wa nani anaweza kutoa msaada unaohitajika. Hii inahitaji kazi kubwa zaidi na kinachoweza kufanyika wakati wa zoezi hili ni kuunda kikundi ambacho kitafanya kazi ya kujenga mahusiano na hizo taasisi ambazo zitahitajika ili kuleta hayo mabadiliko yanayotarajiwa hapo baadaye.

19. Jedwali mlinganisho (Spectrum lines)

Madhumuni
Kujadili na kutafuta habari kuhusu suala linalojadiliwa kwa kuonesha wapi ipo kwenye mtiririko unaoanzia ; kutokuwapo, uchache hadi uwingi, au udogo hadi ukubwa.
Kukusanya maoni kuhusu mtazamo wa washiriki kuhusu suala fulani.

Mbinu

Hii ni kati ya mbinu zilizo rahisi kutumia. Majadiliano yanatazama msitari mmoja ambao unawakilisha, kutokuwapo kwa kitu kinachozungiziwa hadi kuwapo kwa wingi.

Kuna aina mbili za mistari ya spectum.

Ya kwanza ni pale ambapo mnajadili suala fulani kwa kutumia msitari kama kiwakilishi cha maoni yenu ambapo mwisho wa msitari kwa pande zote mbili imepewa thamani maalum. Kwa mfano; miaka kati ya 0 hadi 100, mahari yaliyolipwa kati ya ngombe 0 hadi 20+, na umbali wa kutembea kwenda kwenye chanzo cha maji wakati wa kiangazi.

Suala	Spectrum / Kiasi
Umri wa mtoto wako wa kwanza	Miaka 0 0 miaka miaka 50 +
Mahari ya juu uliyowahi kulipa	Ng'ombe 0 0 Ngombe Ng'ombe 20 +
Umbali wa kufika chanzo cha maji	Kilomita 0 0 Kilomita Kilomita 30 +

Ya pili ni pale ambapo mnatoa maoni, hisia, mtazamo, kuhusu suala fulani kwa kutumia msitari kama kiwakilishi cha maoni yenu ambapo mwisho wa msitari kwa pande zote mbili haina thamani maalum ila inaonyesha hali mbili amabazo ni tofauti kabisa.

Suala	Spectrum / Kiasi
Uwezo wa kuchagua chakula ninachopenda	Uwezo wangu ni Mdogo sana Mkubwa sana
Ufugaji wa kondoo kwenye sehemu za baridi.	Ufugaji kondoo Sipendi Ninapenda Ninapenda sana
	Kilomita 0

Ni muhimu kujua ni aina gani ya zoezi ambalo unataka fufanya. Kama utazungumzia suala ambalo unachotaka kupima utatumia ama nambari utahitaji kuwe thamani ambazo zinaendana na majibu unayotegemea kupata kutoka kwa washiriki. Kwa mfano kama unauliza ni mara ngapi mtu anakula chakula kwa siku, idadi ya juu utakayoweka katika majibu unayotegemea kupata itakuwa ni ngapi?

Kama ukiuliza ni maboma mangapi unatembelea kwa siku, kuna hatari ya kuweka namba ambayo ni ndogo kuliko idadi ambayo watu wengine wanatembelea kwa siku. Uchaguzi wa majibu unaoanzia *maboma machache kuliko ambavyo ningetaka* na *maboma mengine mno kuliko ambavyo ningetaka* inauliza suali ambalo ni tofauti kwa kuwa linaangalia jinsi mtu anavyofikiri na kusikia kuhusu kutembelea maboma.

Matumizi ya kuweka alama kwenye sehemu ya msitari kama kiwakilishi cha maoni ya washiriki inatoa nafasi kwa mhamasishaji kuuliza washiriki ni kwa nini wameweka alama kwenye sehemu moja ya msitari na siyo kwenye sehemu ingine. Unaweza kuendelea kuuza ni nini kingehitakji kubadilike ili aweze kuweka alama kwenye upande mwingine wa msitari. Kuzungumzia alama iliyo kwenye inarahisisha majadiliano kuhusu masuala ambayo yangeonekana kuwa nyeti kama kwa mfano ukosefu wa chakula, na ufukara katika kila kaya.

Kutazama historia: Baada ya washiriki kuweka alama ya pale alipo kwenye msitari, unaweza ukatazama mwelekeo kwa miaka iliyopita kwa kuwaambia waweke alama inayoonyesha kwamba kwa mwaka uliopita hiyo alama wangeiweka wapi. Kufuatana na suala linalozungumziwa, inawezekana pia kuuliza kwa miaka mingine iliyopita hali ilikuwaje.

Inawezekana pia kutazama hata kwa wakati ujao kuwa. Unafikiri utaweka wapi alama hii kwa mwaka au mwezi unaokuja. Hii ni njia ya kuangalia mategemeo ya washiriki kwa wakati ujao. Mlevi wa gongo kwa mfano anaweza akaweka alama karibu na mwisho wa msitari inayoonesha kuwa kunywa gongo mara chache sana kwa mwaka hata ingawaje anaona vigumu kukubali kuwa anataka kupunguza unywaji wa pombe ya gongo.

20. Mpambano wa nguvu za kuendesha na za kuzuia

Madhumuni:
Kuchunguza uwezekano wa kutekeleza au kuharakisha utekelezaji wa shughuli yeyote ile kufuatana na maoni ya washiriki.

Kuanzisha mjadala kuhusu matatizo yaliyopo, ili kuchunguza jinsi gani yanavyoweza kutatuliwa. Ni matatizo gani ambayo hayawezi kutatulika?

Nyenzo hii unachukulia kuwa katika utekekelezaji wa shughuli yeyote ile kuna nguvu za aina mbili, zile zinazoendesha shughuli hiyo kufanyika na zile ambazo zinazuia shughuli hiyo kufanyika na uwiano wa nguvu hizi katika mpambano ndio unasababisha mabadiliko kutokea.

Nguvu za kuendesha ndizo zinazosukuma shughuli ielekee upande fulani, zinachochea mabadaliko na kuendelea kuyasukuma yaende upande huo. Nguvu za kuzuia ndizo zinazofifisha kasi ya nguvu za kuendesha. Mfano ni kutokuwa na ari ya kazi, chuki, na kutokufanya matengenezo ya vifaa. Nguvu za kuendesha zinapoimarika na kuwa sawa na nguvu za kuzuia, shughuli inaweza kuendelea, ila pindi zinapopungua na kuzidiwa na nguvu za kuzuia shughuli inasimama.

Mbinu:

Eleza kuwa tatizo ni kukwama katika utekelezaji wa shughuli, ama kufanya mabadiliko au kuboresha ufanisi.

Itasaidia sana kama ukiweza kupata kielelezo cha tatizo, na washiriki wakusaidie kukitengeneza. Inaweza ikawa ni gari limeharibika na watu wanalisukuma kutoka pande zote mbili, ngombe amekwama kwenye tope la bwawa linalokauka na watu wanajaribu kumvuta na tope nalo linamshikilia chini.

Washiriki wajadili na kuandika kwenye karatasi mambo yale yanayofanya iwe rahisi kupata/ kufanikisha mabadiliko, na halafu pia wajadili na kuandika kwenye karatasi lingine, mambo yale yanayofanya iwe ni vigumu kufanikisha kile kinachofanyika. Kila karatasi libandikwe kwenye upande mmoja wa tatizo unaoendana na kile kinachoelezewa.

Washiriki waulize masuali wapate kuelewa vizuri, na wakitaka wafanye mabadiliko.

Waambie washiriki wapime umuhimu wa mambo waliyoyataja. Yale yaliyo na nguvu kubwa zaidi wa kuzuia, yawekwe karibu na tatizo na yaliyo na uwezo mdogo zaidi ziwekwe mbali na tatizo. Kwa upande mwingine wa tatizo, yale yaliyo na uwezo mkubwa zaidi wa kufanikisha ufanisi wa shughuli hiyo ziwekwe karibu zaidi na tatizo na yale yenye uwezo mdogo yawekwe mbali na tatizo.

Washiriki wahamishe makaratasi yenye mambo yaliyoandikwa kama wanavyotaka.

Ikiwa washiriki wanaridhika kuwa mchoro unaonyesha mambo yanayofanikisha na kukwamisha ufanisi wa shughuli, sehemu ya kwanza ya zoezi itakuwa imekamilika.

Inawezekana kuendelea kuuliza zaidi kuhusu mambo yaliyoandikwa; ni jinsi gani hili au lile linaweza ama kupunguzwa nguvu/ uwezo wake au kuimarishwa iwe na nguvu au uwezo zaidi.

Inawezekana kutumia mchoro uliopo kuongezea maelezo zaidi chini ya kila jambo lililotajwa; yanayoweza kufanyika ili kuleta mabadiliko, badiliko lipi litahitaji raslimali nyingi zaidi, badiliko lipi litahitaji muda mwingi zaidi, badiliko lipi litakuwa na manufaa makubwa zaidi na chochote kile ambacho unadhani ni vizuri kukiulizia.

Ni vizuri kuangalia kama mahali ambapo kuna mambo mawili ambayo yanapingana, na ambapo kuna mvutano, k.v madiwani wengine wanaunga mkono na wengine na wanapinga.

Ni vizuri pia kuona kama kuna mambo ambayo hayana kipingamizi, ni nini tunachoweza kufanya ili kuongeza ufanisi.

21. The Prisoners Dillema

Madhumuni.
Kubadilishana maoni kuhusu kujenga imani.
Kubadilishana mawazo kuhusu kufanya kazi katika vikundi.

Mbinu

1. Eleza kuwa nataka kuwashirikisha katika zoezi ambalo litahitaji wajigawe katika makundi mawili madogo.

   Kiasi ambacho utaelezea madhumuni ya zoezi inategemea sana Unaweza ukaeleza kwa kifupi kuwa inaonesha mawazo ya kufanya kazi pamoja, ushirikiano na kwamba baada ya zoezi utaeleza maana yake halisi.

2. Oneshe kwa vikundi vyote viwili alama ambazo itabidi kila mmoja achagua ni ipi anaipendelea. Hakikisha kuwa alama zote mbili zinaeleweka na kuwa hakuna alama ambayo ina maana yeyote maalum kwa washiriki. Katika zoezi hili tutatumia alama ya rangi za bluu na nyekundu.

   Kila kikundi kitaambiwa kichague alama moja.

3. Elezea matokeo ya zoezi yatakuwa ni nini na zawadi ambazo zitatolewa kwa kila kikundi kufuatana na uchaguzi ambao wanaufanya. Kuna mamambo matatu ambayo yanaweza kutokea.
   a) Kama vikundi vyote vitachagua nyekundu, kila kikundi kitazawadiwa xx viwili.
   b) Kama vikundi vyote vitachagua bluu, kila kimoja kitapewa x kimoja.
   c) Kama kikundi kimoja kitachagua nyekundu na kingine kikachagua bluu, kikundi kilichochagua blue kitapewa xx tatu na kilichagua nyekundu hawatapata kitu.

Kikundi 1	Zawadi		Kikundi 2
1. Nyekundu	2	2	Nyekundu
2. Bluu	1	2	Bluu
3. Bluu	3	0	Nyekundu
Nyekundu	0	3	Bluu

Mshiriki mmoja awaeleze wengine ili kuhakikisha kuwa wanaelewa.

4. Kila kikundi kikae mbali kidogo na kingine ili kisiweze kusikia wenzake wakizungumza na kujua wanachagua nini.

   Kila kikundi kiwe kimepewe alama karatasi mbili, moja yenye (duara katikati na kuwekewa rangi) alama nyekundu na ingine yenye alama ya bluu. Kila kikundi kiamue ni rangi wanaichagua/ au wanaicheza.

5. Kila kikundi kitume mwakilishi wao mbele kuwasilisha kwako alama waliyoichagua. Angalia alama kila kikundi ilichochagua na utoe zawadi kufuatana na makubaliano.

6. Eleza kuwa utarudia zoezi hilo mara kadhaa. Usiweke wazi kuwa utairudia mara ngapi bali ielewekae kuwa ni mara nyingi. Washiriki waelewe kuwa angalau mchezo utaendelea angalau mara kumi.

7. Waite tena wawakilishi wa kila kikundi na alama waliyoichagua na na baada ya kuzitazama utoe zawadi kama inavyostahili. Endelea na zoezi hili mpaka ifikie kiasi ambacho unafikiri imetosha.

8. Wakati mchezo unaendelea itakuwa ni vizuri kama ukiwaita wawakilishi wa vikundi vyote viwili na kuwaambia wajadili na kuona kama wanaweza kuafukiana kuhusu uchaguzi wa rangi ya kucheza kwa namna ambavyo itanufaisha pande zote mbili.

   Unaweza pia ukaitisha mkutano wa washiriki wote ili wote wajadiliane na kuona kama wanaweza kuafikiana.

   Mkutano wa washiriki wote uitishwe pale ambapo vikundi vyote haviheshimu maafikiano (kila kukindi kinachagua rangi ya bluu mfulilizo).

9. Unapoona kuwa hakuna tena ambacho washiriki wanaweza kujifunza tangaza kuwa uchaguzi unaofuata ndio utakuwa wa mwisho. Waite wawakilishi kwa mara mwisho utoe zawadi za kila kikundi na uwaite washiriki wote kwa pamoja ili wabadilishane mawazo kuhusu mchezo huo.

Upatikanaji wa Maji



Ugonjwa wa Chambavu




James amechelewa kufika kwa siku mbili
Alikwenda Arusha
Kununua samani
Samani ni rahisi zaidi Arusha
Ni vigumu kufanya kazi bila samani
Ofisi za kata hazina samani
Anahitajika mhusika akafanye malipo
Unahitaji kulipa fedha za kuhifadhiwa fanicha Arusha
Samani iko tayari kuchukuliwa
Samani ilitengenzwa kama ilvyoahidiwa
Mamlaka ya Hifadhi walichukua fanicha yao
Huwezi kupata fedha kutoka shirika lingine.
Hawatoi huduma ya kutunza mizigo.
?
Mamlaka ya hifadhi wanataka samani yao waipeleke kwingine

22. Kalenda ya Msimu

Madhumuni

- Kalenda za misimu ni mbinu nzuri ya kuonesha mabadiliko ya katika vipengele mbalimbali vya maisha (kv. Mvua, maji, malisho ya mifugo, bei za mazao ya chakula, mifugo, wingi wa kazi kwa vijana, wanawake, vijana, matumizi ya fedha n.k.) yanayotokea katika kipindi cha mwaka au msimu.

- Inasaidia kubainisha mabadiliko yanayotokea kila mara kufuatana na msimu haya yanasaidia kueleza ni kwa nini katika kupindi fulani mabadiliko katika hali ya hewa yanakuwa na athari fulani katika hali ya maisha ya wanakijiji, na katika vipindi vingine hali hewa inaleta neema katika maisha ya wanakijiji. Mabadiliko haya ya kimsimu ni muhimu katika kuelewa ni kwa nini katika kipindi fulani kuna hali fulani kama vile uhaba au wingi wa mvua, malisho ya mifugo, chakula, fedha, maradhi ya mifugo na hata binadamu, n.k. Hali ya makundi mbalimbali katika jamii vilevile hubadilika kufuatana na misimu ya mwaka.

- Hubainisha ni katika vipindi gani matatizo kadhaa au neema Fulani hupatikana. Baada ya kuelewa kiini cha matatizo kwa kuhusisha na mabadiliko ya misimu ya mwaka, inakuwa ni rahisi zaidi kupanga ni nini kinaweza kufanyika ili kupunguza makali ya athari za mabadiliko hayo kwa kaya au kundi fulani la jamii.

Mbinu

- Chagua eneo ambalo lina nafasi ya kutosha chini kwa kikundi kutengeneza mchoro kwenye udongo. Tumia kijiti kuchora kwenye udongo ama mchanga na unaweza kupanga mawe madogo madogo, vijiti, majani, mavi ya mbuzi, n.k. Kama utachora kwenye karatasi kubwa, na ni muhimu uhakikishe inaenea kwenye ukurasa mmoja tuu!

- Anza kwa kuchora msitari ulionyooka kwenye eneo lililoandaliwa, na ueleze kuwa msitari huo unawakilisha mwaka mzima. Waambie washiriki waugawanye huo katika miezi, au misimu ya mwaka kufuatana na vile wanachoona kuwa itafaa zaidi. Mgawanyo huu uoneshwe juu ya ule msitari mrefu uliochorwa.

- Anza na kipengele kilicho rahisi zaidi kueleweka. Kwa mfano waeleze ni kipindi gani ambacho wanapata mvua nyingi zaidi na uionyeshe kwenye kalenda kwa kuweka mawe mengi zaidi, msitari mrefu zaidi.

- Baada ya kipengele hicho cha mvua, endelea na kujadili vipengele vingine muhimu kama vile makisho ya mifugo, upatikanaji wa chakula/ maziwa, magonjwa ya mifugo, magonjwa ya binadamu, n.k.

- Michoro hii pia ifanywe na vikundi vingine k.v. wanawake, vijana, wazee, wafugaji, wakulima n.k. ili kujua tofauti muhimu katika makundi haya.

- Siyo lazima kalenda ianzie mwezi Januari, inaweza ikaanzia kipindi chochote ambacho washiriki wanaona kuwa ndipo msimu wa mwaka unaanza.

Ni muhimu michoro hii ioneshe mabadiliko yanayotokea katika kipindi cha mwaka au msimu, kwa kipengele hicho kinachozungumziwa.

Maelezo yatakoyotolewa latika majadiliano ya kalenda ya msimu yatasaidia pia kubainisha maoni na mtazamo wa washiriki kuhusu masuala mbalimbali yakiwamo;

- Mgawanyo wa shughuli za kazi za uzalishaji na za ndani kati ya wanaume na wanawake.
- Matumizi na umiliki wa amali mbalimbali za kaya hasusan chakula.
- Kiwango ambacho jamii inategemea sana asili mali iliyopo kijijini kupata mahitaki yao,
- Nini zao gani wanakijiji wanategemea kwa chakula ambalo lazima lipatikane au lioteshwe wakati wote.
- Jinsi inavyoyaona matatizo yake na kupima fursa zilizopo za kuyatatau

Kalenda ya msimu - Kakesio




maharage
beans
maharage
karanga
Baada ya mavuno kausha
safisha anika
Kazi
kwa
Muda
wote
Njaa
Kulima
Kazi
Nyepesi
kulima
kupanda
Viazi vitamu
kuvuna
kupanda
kupanda
palizi
kuvuna
Kazi ya ndani
ususi pika & uza pombe
kulima
kupanda
Viazi vitamu
Safisha shamba
Aug
Sep
Oct
Nov
Dec
Jan
Feb
Mar
Apr
May
Jun
Jul

23. Shughuli za kila siku

Madhumuni

Uchambuzi wa mtiririko wa shughuli za kila siku unasaidia kubainisha shughuli mbalimbali zinazofanywa na makundi mbalimbali katika jamii.

Uchambuzi huu unasaidia kuonesha wingi na uzito wa shughuli ambazo kundi fulani, kama vile wanawake, wanaume, kaya zenye uwezo mdogo, vijana, wazee, kaya zenye uwezo mkubwa wa mali wanafanya kwa siku nzima.

Mbinu
Andaa vikundi tofauti vya wanawake na wanaume. Hakikisha kuwa kila kikundi kina washiriki kutoka makundi mbalimbali ya jamii.

Eleza kuwa unataka kila kikundi kijadili na kuonesha shughuli mbalimbali ambazo wanazifanya kwa kawaida kuanzia asubuhi hadi jioni. Itakuwa ni rahisi zaidi kama washiriki watatazama shughuli walizofanya jana yake. Wapate mtiririko wa shughuli kwa siku nzima huku wakionesha kuwa kila shughuli inachukua muda gani.

Unaweza kuchora mduara wa saa na kuutumia kuonesha muda ambao kila shughula inachukua. Unaweza pia ukachora msitari ulionyooka na kuugawanya kwa masaa ishirini na manne na kuonyesha ni wakati gani ambao kila shughuli inafanyika. Michoro hii inatoa kwa haraka sura ya uwingi na uzito wa shughuli ambazo zinaikabili kila kikundi.

Shughuli ambazo zinafanyika kwa wakati mmoja kama vile kwa wanawake kunyonyesha mtoto na kupika chakula ziwekwe kwenye sehemu mmoja.

Baada ya kuukamilisha mchoro wa kwanza, kutegemea ni msimu upi (kiangazi au masika), itakuwa ni vizuri washiriki wakitengeneza mchoro mwingine unaobainisha shughuli zao kwa siku nzima katika msimu mwingine.

Uchambuzi
Baada ya vikundi kutengeneza michoro inayoonesha shughuli zao kwa kila siku itakuwa ni vizuri kujadili masuala yafuatayo ili kusaidia kufanya uchambuzi;

- Kwa kila mtu/kundi angalia mgawanyo wa muda ukoje kwenye shughuli za; kuzalisha, ndani ya nyumba, jamii, mapumziko, na kulala, na shughuli hizi sinapishana vipi na zile za vikundi vingine kwa kila msimu.
- Je kila mtu ana shughuli nyingi sana za kufanya au wengine wana chache zaidi.
- Je shughuli za wanawake zinatofautiana vipi na zile za wanaume?
- Ni kikundi gani ambacho kina shughuli nyingi zaidi.
- Shughuli za makundi mbalimbali za jamii zinatofautiana vipi?

Uchambuzi wa shughuli za siku

Kikundi cha Wanawake

Kipindi cha Kiangazi



Kikundi cha Wanawake

Kipindi cha Kiangazi



Kikundi cha Wanawake

Kipindi cha Kiangazi

11.00
11.00

Wanawake - Matumizi ya Muda, Msimu wa Kiangazi



Kikundi cha wanawake

Msimu wa Kiangazi

Muda	**Shughuli**
12.00	Kuamka na kukamua ngombe
1:00	Kuwasha moto, kupika na kuwapa watoto chakula
2:00	Watoto kuwatenganisha ndama na mama zao
3:00	Ngombe na mbuzifugo kuondoka kwenda malishoni
4:00	Kwenda kutafuta kuni
5:00	kutafuta kuni
6:00	Kurudi kutoka kutafuta kuni
7:00	Kupumzika
8:00	Kwenda kuteka maji
9:00	Kwenda kuteka maji
10:00	Kurudi kutoka kuteka maji, Kuandaa vibuyu kwa ajili ya kukamua ngombe
11:00	Kungoja mifugo irudi kutoka malishoni
12:00	Lufungia ngombe na mbuzi ndani ya boma na kuangalia kama wamerudi salama
1:00	Kukamua ngombe
2:00	Kuandaa chakula
3:00	Kuwapa watoto chakula
4:00	Kulala

Kikundi cha wanawake
Msimu wa Kiangazi

Muda	**Shughuli**
10:00	Kuamka na kuwasha moto
11:00 –12:00	Kuamka na kukamua ngombe
1:00	Kufungua boma la ngombe na kufagia eneo la ndama kukaa.
4:00	Watoto kuwatenganisha ndama na mama zao ili waende malishoni
4:30 –6:00	Kutengeneza siagi kutokana na maziwa
7:00 – 9:00	Kupumzika
10:00	Kusiliba nyumba na mavi ya ngombe ili kuzuia mvua. Mbuzi wanaanza kurudi toka malishoni
11:00	Kuandaa vibuyu kwa ajili ya kukamua ngombe Ngombe kuanza kuwasili
12:00	Kufungia mlango wa ngombe
1:00- 4:00	Kukamua ngombe Kunywa maziwa
4:00	Wazee kulala Vijana kucheza pamoja hadi saa ya kulala saa tano na nusu
5:15	Kulala

24. Historia ya Jamii

Madhumuni
Kupata habari za historia ya jamii, hususan siku za nyuma/ imetoka wapi, ni muhimu ili kutusaidia kuelewa imefikaje hapa ilipo, na kwamba kutoka hapa inawezaje kuendelea mbele.

Inaangalia kwa undani matukio mbalimbali katika ngazi ya kimataifa, kitaifa, mkoa na wilaya na jamii, ambazo jamii inaona ni muhimu katika historia yake, na ambayo yanasaidia kuelewa umililki na matumizi ya raslimali katika jamii.

Kurekodi matukio muhimu katika historia ya jamii ambayo yamekuwa tuu yanasimuliwa na pengine hadi sasa hayajaandikwa popote.

Kuchochea majadiliano kuhusu matatizo na mafanikio katika jamii kwa kipindi kilichopita kwa kadiri ambavyo wazee wanaweza kukumbuka, kama walivyoelezwa na wazazi na babu zao. Majadiliano haya yanatoa nafasi ya kuuliza wazee jinsi matatizo kama haya zamani yalivyotatuliwa na jamii na kuangalia ni jinsi gani jamii inaweza kujufunza kutokana na mbinu hizo za utatuzi.

Mbinu
Majadiliano yajumuishe wanakijiji wakiwapo wazee wanaume na wanaume, vijana, na viongozi wa taasisi mbalimbali za kimila na za maendeleo, msisitizo ukiwa kwa wazee na wale walioishi katika eneo hilo kwa muda mrefu zaidi.

Kama washiriki ni wengi, wagawanywe katika vikundi vidogo vidogo ambavyo vitafanya majadiliano na baada ya majadiliano vitakutana kufanananisha yale ambayo kila kikundi imepata.

Majadiliano katika vikundi ni mbinu nzuri zaidi kuliko kuzungumza na mtu mmoja kwa kuwa inasaidia kuulizana na kukumbushana.

Mwezeshaji asisitize kuwa washiriki waangalie matukio muhimu ambayo yamechangia sana katika jamii kufikia hapa, shughuli mbalimbali za jamii kuanzishwa, na hata kuwapata na viongozi mbalimbali.

Kwa kutumia kijiti na kuandika kwenye udongo, au kwenye flip chart, anza kwa kuuliza masuala yafuatayo:

- Lini kijiji kilianza na nani walikuwa waanzilishi?
- Tukio muhimu la kwanza unaloweza kukumbuka ni lipi?
- Kama kumekuwa na uhamiaji au uhamaji mkubwa kwenye kijiji hiki/ unafikiri ni kwa nini?

Washiriki waendelee na kujadili matukio muhimu yaliyotokea kwa kuanzia na yale ya zamani zaidi hadi kufikia miaka ya karibuni. Mjadala huu unaweza ukawa unatazama kipindi cha miaka kumi kumi au mitano mitano.

MATUKIO MUHIMU KATIKA HISTORIA YA HIFADHI YA NGORONGORO

1959 Hifadhi ya Ngorongoro iliundwa baada ya kutenganishwa na Hifadhi ya Serengeti. Wamasai walihama kutoka ndani ya Serengeti

1965 Kulipuka kwa volcano ya mlima Lengai

1973 Ukanme mkumbwa ambayo iliua wanyama na mifugo mingi.

1975 Wamasai walihamishwa kutoka ndani ya crater ya Ngorongoro

1975 Kilimo kilipigwa marufuku

1975 Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Hifadhi

1987 Uwizi wa mifugo

1990 IUCN ilifanya utafiti kuhusu Hifadhi ya Ngorongoro kama eneo linaloruhusu matumizi ya hifadhi na mifugo na mengine kwa maendeleo ya wakazi chini ya (GMP) mpango wa kusimamia mendeleo ya hifadhi.

1993 Kilimo kuruhusiwa tena kwenye eneo la hifadhi.

1994 Kuanzishwa kwa Baraza la Wafugaji.

1998 Kuanzishwa kwa mradi wa kusaidia wafugaji maskini Ngorongoro ERETO.